




UKURASA 4

**SIMULIZI** mama wa watoto mapacha wanaokula magodoro




FAO inavyowaondoa wanawake Kigoma kutoka wategemezi, hadi wanaohudumia
• Siri ya majibu iko ndani ya shamba lao

UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Ijumaa Mei 20, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580951

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Spika ambana waziri

UKURASA 2



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

## Wanaume vinara vifo vya UKIMWI

UKURASA 3

UKURASA WA 2

### SAMIA ATANGAZA FURSA YA KIWANDA MKOANI TABORA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka wananchi mkoani Tabora, kuchangamkia fursa za ajira kupitia...



UKURASA WA 4

### VIPAUMBELE VYA WIZARA YA ULINZI 2022/23 HIVI

WIZARA ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeainisha vipaumbele...

UKURASA WA 7

### WENYE ULEMAVU SASA WAKUMBUKWA AJIRA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imetoa kipaumbele kikubwa cha ajira kwa watu wenye ulemavu na kuwataka...




Mwenyekiti wa Bodi ya NMB Foundation, Ruth Zaipuna (wapili kushoto), akizindua rasmi dirisha la kupokea maombi ya ufadhili wa wanafunzi wanaotegemea kuingia kidato cha tano mwaka huu na wale wanaotarajia kuingia vyuo vikuu kwa ajili ya shahada ya kwanza ya masomo, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mjumbe wa Bodi, Juma Kimori (kushoto), Katibu wa NMB Foundation, Consolata Mosha (kulia) na Mjumbe wa Bodi, Filbert Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waandishi wateule IPP wang'ara tuzo EJAT 2021

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA YAITISHA MBEYA KWANZA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Waziri abanwa kujibu maswali mepesi bungeni

**Na Romana Mallya,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amemshukia Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Petrobas Katambi, baada ya kutoa majibu kwamba vijana ambao hawapati mikopo inayotolewa na halmashauri huenda si Watanzania bali ni raia wa Kenya.

Amesema majibu hayo hayaleti picha nzuri na kwamba limewakera vijana wanaohangaika kutafuta ajira na mikopo, hivyo kumtaka arudie kulijibu.

Akizungumza jana bungeni jijini Dodoma Spika, alisema naibu waziri huyo alitoa majibu hayo juzi asubuhi wakati akijibu la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda.

Spika alisema naibu waziri huyo aliulizwa kuhusu mikopo inayotolewa kwa vijana kupitia halmashauri na wakati akijibu, majibu yake yaliashiria vijana wote wenye uhitaji wa mikopo wanapata.

"Majibu hayo hayana uhalisia na wakati akieleza hivyo alikwenda mbali zaidi na kueleza kwamba serikali inachukua hatua na akaeleza mambo ambayo serikali inafanya ili kuhakikisha vijana wanapata ajira pia wanaweza kujiajiri kwa maana alitoa maelekezo ya mafunzo mbalimbali," alisema.

Spika alisema swali hilo lilihusu mikopo na kwamba wako vijana ambao hawapati na serikali ina mpango gani.

"Wakati naibu waziri anajibu hapa alionyesha ishara kwamba vijana wote wenye uhitaji wa mikopo wanapata mikopo na kwamba wapo ambao hawapati mikopo pengine si Watanzania ni Wakenya.

"Waheshimiwa wabunge kwa sababu ni lugha ya mazungumzo inakuwa yale majibu si kwamba ameyaandaa kabla kwa sababu. Ni swali la nyongeza, lakini majibu haya hayajapeleka picha nzuri kwa vijana wetu ambao wanahangaika hapa na pale kujaribu kutafuta ajira lakini kutafuta hiyo mikopo kuboresha shughuli zao ambazo wamezianzisha pengine hawajaweza kuanzisha," alisema.

Alisema majibu ya namna hiyo hayajajibu swali la mbunge ambaye alitaka kujua watasaidiwaje na kueleza kuwa linapaswa kujibiwa upya.

"Ili mheshimiwa waziri apate nafasi ya kurekebisha yale majibu yake aliyoyatoa awali, swali hili litajibiwa upya. Pamoja na kujibiwa upya maneno hayo yameashiria vijana ambao wamekosa mikopo ni wa Kenya si maneno mazuri pamoja na kwamba ni lugha ya mazungumzo," alisema.

"Lazima waheshimiwa wabunge na waheshimiwa mawaziri tutumie lugha ambayo itapeleka ujumbe huko nje bila kuwakatisha tamaa vijana ambao wanajishughulisha na mambo mbalimbali," aliongeza.

Spika alisema hayo yamekuwa yakijitokeza bungeni ndiyo maana huwa wanasisitiza maswali ya nyongeza yaendane na swali la msingi ili kupata majibu mahususi.

Katika hatua nyingine, Spika Ackson alisema katika kipindi hicho cha maswali na majibu siku hiyo, Mbunge Viti Maalum, Husna Sekiboko naye aliuliza swali la msingi kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia akitaka kujua ni hatua zinazochukuliwa kukomesha kuvuja kwa mitihani nchini.

Spika alisema pamoja na mambo mengine naibu waziri alieleza na kunukuu maneno yake: "Mheshimiwa Spika kwanza naomba nimhakikishie mheshimiwa mbunge suala la uvujaji mitihani halipo. Mara ya mwisho mitihani ilivuja mwaka 2008, ulikuwa mtihani mmoja wa somo la hisabati wa kidato cha nne, kutoka mwaka 2008 hakujawahi kutokea uvujaji wa mitihani."

Hata hivyo, spika alisema majibu hayo yalikinzana na taarifa iliyotolewa na kamati ya huduma na maendeleo ya jamii.




Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari (EJAT) 2021, ambaye ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu majina ya wateule wa tuzo hizo. Kushoto ni Mwenyekiti wa Jopo la Majaji wa tuzo hizo, Mkumbwa Ally. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Samia atangaza neema Tabora, fursa ujenzi kiwanda cha asali

**Na Halfani Chusi**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka wananchi mkoani Tabora, kuchangamkia fursa za ajira kupitia miradi inayoendelea mkoani humo.

Pia amewaahidi Mkoa wa Tabora utakuwa alama ya asali ndani na nje ya nchi kupitia kiwanda kikubwa kinachotarajiwa kujengwa mkoani humo.

Aliyasema hayo jana wakati akihitimisha ziara ya kikazi ya siku tatu mkoani humo ambayo ilienda sambamba na ufunguzi wa barabara.

Akiwa mkoani humo, Rais Samia aliwataka wananchi wa mkoa wa Tabora kuwa walinzi wa miundombinu inayojengwa ikiwamo barabara, reli na kiwanda cha kusindika asali kinachotarajiwa kuanza kujengwa hivi karibuni.

Rais Samia alisema Tabora imekuwa miongoni mwa mikoa yenye rasilimali nyingi, hivyo serikali haina budi kupeleka maendeleo mkoani humo.

"Ukiangalia mkoa wa Tabora kuna ardhi ya kutosha kwa kilimo, lakini kuna hifadhi za misitu ambayo imekuwa ikisaidia upatikananji wa asali. Kwa hiyo niseme tu fedha ambazo zimetolewa kwa ajili ya miradi inayoendelea huku zikatumike ipasavyo kwa kuzingatia kanuni na sheria za nchi," alisema.

Katika hatua nyingine, Rais Samia aliwaagiza wakuu wa halmashauri zote nchini kuwa wakweli na wawazi kwa wananchi pindi wanapopewa pesa kwa ajili ya kusimamia miradi.

"Fedha za halmashauri zitumike kwa uwazi lakini inapaswa wananchi wajue ni kiasi gani kimetolewa kwa ajili ya mradi husika na wakijua wataweza kufatilia kwa kuangalia mradi na pesa iliyotumika je inafanania," alisema na kuongeza:

"Kwenye fedha za seriali lazima kanuni za fedha zifuatwe. Pesa za serikali zinahitaji nidhamu siyo za mtu binafsi.

Pamoja na mambo mengine, Rais Samia aliwaahidi wananchi wa Mkoa wa Tabora kumaliza kero mbalimbli zinazowakabili kama inavyosema ilani ya uchaguzi.

# Waandishi wateule wa IPP wang'ara tuzo za EJAT 2021

**Na Maulid Mmbaga**

WAANDISHI 15 wa IPP Media wameng'ara kwa kuwa miongoni mwa wateule 60 wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2021, zinazoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Katika tuzo hizo wateule wa Nipashe ni saba, The Guardian watano na ITV watatu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT, Kajubi Mukajanga, alikusanya jumla ya kazi 598 za kuwania tuzo 20 zilipitiwa na jopo la majaji saba na kupata wateule hao.

Waandishi wa IPP Media waliobuka ni Agusta Njoji, Sanula Athanas, Sabato Kasika, Mary Geofrey, Marco Maduhu, Elizabeth Zaya na Halfani Chusi wa gazeti la Nipashe.

Kwa upande wa The gazeti la The Guardian ni Muhudini Msamba, Francis Kajubi, Beatrice Philemon, Jenifer Gilla na Christina Mwakangale. Kwa ITV ni Peter Rodgers, Masekepa Masekepa na Jackline Silemu.

Waandishi wa vyombo vingine walioteuliwa na idadi yao kwenye mabano ni Zanzibar Leo (8), Mwananchi (7), Uhuru (1), Habari Leo (1), The Citizen (1), Jamhuri (1), Star TV (4), TBC (1), Azam TV (1), ZBC FM (1), Zanzibar Cable TV (1).

Wengine ni UFM Radio (2), Dar24 online TV (2) na The Chanzo online (2), Shamba FM (1), City FM (1), Highlands FM Radio (1) na CG FM Radio (1), TIFU TV Online (1), Watetezi online TV (1), Nukta.blog (1) na BBC Swahili Online (1).

"Jopo hilo lilitumia siku tisa badala ya nane kutokana na ongezeko la kazi 202 kutoka tuzo za EJAT 2020, ambapo kazi 396 ziliwasilishwa ukilinganisha na kazi 598 za sasa, niwapongeze majaji na kwa kazi kubwa waliyoifanya usiku na mchana ya kupitia kazi hizo," alisema Mukajanga.

Aliongeza kuwa katika wateule hao, wanawake ni 28 sawa na asilimia 47 ikiwa ni ongezeko la asilimia tatu, ikilinganishwa na mwaka uliopita walikuwa 26 sawa na asilimia 44. Aidha, alisema wanaume wateule kwenye tuzo hizo ni 32 sawa na asilimia 53.

Pia, alieleza kuwa kwa mujibu wa majaji, kazi za mwaka huu zimeonyesha kuwa na kiwango cha juu, ikiwamo waandishi wa mtandao kuonyesha kukomaa katika kazi zao na mwamko wa kushiriki tuzo hizo.

Alibainisha kuwa wanatarajia Rais Samia Suluhu Hassan atakuwa mgeni rasmi katika shughuli za utoaji wa tuzo na ndiye atakayemkabidhi tuzo mshindi wa jumla na wa tuzo ya Maisha ya Mafanikio Katika Uandishi wa Habari (LAJA) 2022. Aidha, alifafanua kuwa tuzo hizo zitatolewa Mei 28, mwaka huu, mkoani Dar es Salaam, ikiwa ni mara ya 13 kuwatunza waandishi waliofanya vizuri katika kazi zao za kiuandishi katika mwaka uliopita.

"Baraza linapenda kuwataarifu waandishi wa habari kuwa katika tuzo za mwakani mfumo wa ujazaji fomu utakuwa ni kwa njia ya mtandao (online) ambapo fomu zitajazwa na kutumwa kwa mtandao. Hii itapunguza matumizi ya karatasi na changamoto za CD kukwama kucheza wakati majaji wanapitia kazi," alisema Mukajanga.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Jopo la Majaji, Mkumbwa Ally, alibainisha changamoto mbalimbali walizokutana nazo wakati wanapitia kazi za waandishi, ikiwemo baadhi ya CD kukwama na kutosoma vizuri, hivyo kusababisha shida katika kusikiliza ili kupata kile wanachokihitaji.

Nyingine ni baadhi ya waandishi walifanya makosa katika ujazaji wa fomu hali iliyosababisha wao kushindwa kujua kazi imefanyika kutoka chombo gani na imefanywa na nani huku kazi moja ikifanana na iliyotoka vyombo viwili tofauti.

"Stori nyingi zilikosa namna ya uwasilishaji kuanzia mwanzo wa stori hadi katikati majaji bado walikuwa hawajui mwandishi amelenga nini na baadhi ya waandishi walikuwa hawazingatii vigezo vya kiuandishi kama kupeleka kazi iliyokwisha shiriki miaka iliyopita na kutohoa kazi za waandishi wengine," alisema Ally.

# Wanaume vinara vifo vya UKIMWI

**Na Sanula Athanas,** MOROGORO

WATU 54,000 nchini wamepata maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) nchini kwa mwaka 2021 huku ripoti mpya ikibainisha kupungua kwa maambukizi hayo kulinganishwa na mwaka 2020 ambao watu 68,000 walipata maambukizi mapya.

Hayo yalibainishwa jana mjini Morogoro na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, aliporejeshwa ripoti mpya ya zilizotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Ukimwi HIV/AIDS (UNAIDS).

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa semina kwa wahariri na waandishi wa habari, Dk. Maboko alisema ripoti mpya inaonyesha juhudi zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau kukabiliana na VVU/UKIMWI zimekuwa na matokeo chanya.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo alisema bado kunahitajika nguvu zaidi ili kuzuia maambukizo mapya ili kupunguza kasi ya maambukizo.

Dk. Maboko alibainisha kuwa vifo vitokanavyo na UKIMWI nchini vimepungua hadi 29,000 mwaka 2021 kutoka vifo 32,000 mwaka uliotangulia, yaani 2020.

"Ukiangalia takwimu za vifo, wanaume wanaoongoza wakati wanawake wanaoongoza kwa maambukizi. Hii ina maana kwamba wanaume wako nyuma kujitokeza kupima na wako nyuma kutumia ARVs (dawa za kupunguza makali ya VVU).

"Wanawake ni wepesi kupima na wanatumia vizuri dawa. Tunamshukuru Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) amekubali kuwa balozi wa wanaume kuhamasisha upimaji kujua hali ya maambukizi ya VVU," alisema. Hata hivyo, mkurugenzi huyo alipotakiwa kuweka wazi takwimu za uwiano halisi wa vifo vya wanaume na wanawake vitokanavyo na UKIMWI, alisita kwa ufafanuzi kwamba: "Ripoti kamili itatangazwa baadaye".

Alisema malengo ya Tanzania ya 95-95-95, kwa maana ya asilimia 95 yapime kujua hali zao kiafya, asilimia 95 wanaobainika kuambukizwa waanze kutumia dawa na asilimia 95 wawe wamepunguza makali ya virusi, yanatekelezwa vizuri ili kulifikia lengo kuu la kudhibiti janga 'HIV/AIDS Epidemic Control' kufikia mwaka 2030, ambao ni ukomo wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Dk. Maboko alisema makadirio mapya yanaonyesha vijana wanaendelea kuwa kundi lililo hatarini zaidi dhidi ya VVU/UKIMWI, hivyo programu nyingi sasa zimeelekezwa kwa kundi hilo.

Alisema ili kudhibiti kuenea kwa virusi, watu wote wanapaswa kupima kujua hali ya maambukizi na wanaobainika kuwa na maambukizi waanze kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU.

"Kama watu hawajui hali zao kuhusu VVU, hawawezi kujikinga wao wenyewe, familia zao, wenzao wao. Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI yalianza miaka mingi iliyopita lakini hayajafanikiwa kufikia lengo kutokana na vikwazo mbalimbali, ukiwamo unyanyapaa, mtazamo hasi dhidi ya VVU/UKIMWI, kutokuwa na elimu kuhusu suala hilo na kutotumia dawa," alifafanua.

**HALI ILIVYO**

Nyangusi Laiser, Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini TACAIDS, akirejea takwimu za kitaifa na kimataifa, alibainisha kuwa kwa mwaka 2020, kulikuwa na watu milioni 37.7 waliokuwa wanaishi na VVU duniani.

Kati yao, watoto wenye umri chini ya miaka 15 ni milioni 1.7 na kwamba asilimia 53 ya waliokuwa wanatumia dawa za kupunguza makali ya virusi walikuwa wanawake. Alisema maambukizi mapya kwa mwaka 2020 yalikuwa watu milioni 1.5, kukionekana kuwapo kupungua kutoka watu milioni tatu mwaka 1997.

"Takwimu zinaonyesha kila siku takriban watu 4,000 huambukizwa VVU duniani na kati yao, 2,400 (asilimia 60) ni waliopo kusini mwa Jangwa la Sahara," alibainisha.

Kwa Tanzania, ofisa huyo alisema kuwa kwa mwaka 2020, watu waliokuwa wanatumia dawa za kupunguza makali ya virusi walikuwa milioni 1.6. Kati yao, wanawake ni milioni moja na wanaume 600,000.

"Maambukizi mapya mwaka 2020 nchini yalikuwa watu 58,000. Kati yao, 37,000 ni wanawake, wanaume 21,000 na ndani ya makundi hayo kuna watoto wenye umri chini ya miaka 15 wapatao 10,000. Vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 24 wanaongoza kwa maambukizi mapya wakiwa asilimia 80 kwenye idadi hiyo ya watu 58,000 waliopata maambukizi mapya.

# Mbaroni tuhuma kumfanyia ukatili wa kingono mjukuu

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa, linamshikilia Desderia Mbwelwa (56), mkulima wa Lumuli Wilaya ya Iringa kwa tuhuma za kumfanyia ukatili wa kingono mtoto wa miaka minane.

Mtoto huyo mwanafunzi wa darasa la tatu alikamatwa na mwanamke huyo na kuvutwa vichakani kisha kumlazimisha afanye tendo la ngono.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa kitendo hicho kilimsababishia mtoto huyo maumivu makali sehemu za siri.

Alisema tukio hilo lilitokea Mei 8, mwaka huu, majira ya saa 10 jioni, na tayari mtuhumiwa huyo amekamatwa na atafikishwa mahakamani upelelezi ukikamilika.

Wakati huo huo, watu watatu walikamatwa katika nyumba za kulala wageni mjini Iringa kwa tuhuma za utapeli, akiwamo Joseph January (28) maarufu kama Mgawe, aliyejifanya mganga wa kienyeji wa kusafisha nyota ya bahati kwa kumwingizia dawa mwanamke kwa kutumia sehemu zake za siri.

Kamanda Bukumbi alisema watuhumiwa hao walikamatwa Mei 12, mwaka huu, majira ya saa tatu usiku katika nyumba ya kulala wageni ya Wihanzi na Udzungwa mjini Iringa.

Wengine walikamatwa kwenye nyumba za wageni eneo la Kihesa na Makorongoni, huku akiwataja kuwa ni January ambaye ni mkulima mkazi wa Ubungo jijini Dar es Salaam, Richard Joseph (24) mkulima wa Sumbawanga na Revold Baruti (23), mkazi wa Sumbawanga.

Alisema kuwa watuhumiwa hao walikamatwa na mabunda ya karatasi nyeusi zilizokatwa na kupangwa mfano wa noti za Tanzania na uchunguzi wa awali ulibaini walipanga kufanya utapeli huku wakitumia gari aina ya Mark X yenye namba za usajili T 979 DWN inayomilikiwa na Herieth Khamis, mkazi wa Dar es Salaam.

Alisema katika upekuzi walikuta vipeperushi vya Sharifu Majini, pete za bahati, dawa aina ya Iodine, Vitamin B complex ambayo imechanganywa na maji.


CRDB BANK
*Tunakusikiliza*

## Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba wa Wanahisa

*Mwenyekiti na Wanahisa,*

**Yah: Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba**
Taarifa inatolewa kwamba **Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba** wa CRDB Bank Plc utafanyika siku ya Jumamosi tarehe **21 Mei 2022**, katika **Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC)**, Ukumbi wa Simba na kwa njia ya kidijitali kuanzia saa tatu kamili **(Saa 3.00) asubuhi** kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuridhia Dondoo.**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Sita.**
4. **Kujadili yatokanayo na kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Sita.**
5. **Kujadili na kupokea Ripoti ya Wakurugenzi wenye dhamana ya Uongozi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2021.**
   5.1 Ripoti ya Wakurugenzi wenye dhamana ya Uongozi.
   5.2 Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2021.
   5.3 Gawio kwa mwaka 2021.
6. **Kuidhinisha ada ya Wakurugenzi.**
7. **Kuteua Wakaguzi wa Hesabu.**
8. **Kuchagua Wajumbe wa Bodi**
   8.1 Wajumbe watatu (3) wa Bodi watakaowakilisha kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja (1%).
   8.2 Mjumbe mmoja (1) wa Bodi atakayewakilisha kundi la wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja na kumi (1% na 10%).
   8.3 Mjumbe mmoja (1) Huru wa Bodi
9. **Kujadili mapendekezo kutoka kwa Wanahisa.**
10. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
11. **Kupanga mahali na tarehe ya Mkutano ujao.**
12. **Kufunga Mkutano.**

***MAELEZO***
1. **Mahudhurio kwa njia ya Kidijitali**: *Mwanahisa anaweza kuhudhuria Mkutano Mkuu kwa njia mbalimbali za kidijitali (SIM Banking, SIM Account na tovuti [https://www.crdbbank.co.tz]). Benki itawatumia wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidijitali.*
2. *Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 13/05/2022 na litafunguliwa tena tarehe 16/05/2022.*
3. *Mapendekezo kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 9 yatumwe na yamfikie Katibu kabla ya* ***Ijumaa tarehe 06/05/2022 saa 10.00 jioni.***
4. *Makabrasha ya Mkutano Mkuu yatapatikana matawini na yanaweza kuchukuliwa kuanzia tarehe* ***10/05/2022****, yatapatikana pia Arusha kwenye ukumbi wa Mkutano tarehe* ***20 hadi 21 Mei 2022****. Pia makabrasha ya Mkutano Mkuu yatapatikana kwenye tovuti ya benki kuanzia tarehe 10/05/2022.*
5. *Wanahisa wanaotaka kuhudhuria Mkutano Mkuu watajigharamia usafiri na malazi.*

**TAARIFA YA SEMINA KWA WANAHISA**
Taarifa inatolewa kwamba kutakuwa na Semina kwa Wanahisa itakayolenga kutoa elimu kuhusu Umuhimu na taratibu za kuandaa Wosia na Mirathi, Kusitisha utoaji wa Risiti za Uwekezaji na Umuhimu wa kulinda Mali zako itafanyika Ijumaa, tarehe 20/05/2022 katika **Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba** kuanzia saa **3.00 asubuhi**.

Kwa mawasiliano tumia anuani ifuatavyo:
**Katibu**
**CRDB Bank Plc**
**CRDB Bank Head Quaters**
**S. L. P. 268**
**Dar-es-Salaam**
**Simu. na. 022 - 2114237, 2117442 - 7 - Fax na. 022 - 2131005**
**Barua pepe –shares_unit@crdbbank.co.tz**

**KWA IDHINI YA BODI**

J. B. Rugambo
**KATIBU**

20 Aprili, 2022

216841202

# Mama wa mapacha wanaokula magodoro afunguka, aomba msaada

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KUNA usemi usemao, ukistaajabu ya Firauni, utaona ya Mussa. Ndivyo unavyoweza kueleza, baada ya mama mwenye watoto wawili mapacha kujitokeza hadharani na kupaza sauti, akiomba msaada wa madaktari bingwa, kujitosa kuwatibu wanawe, wanaokula magodoro badala ya chakula.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Arusha, mama mzazi wa watoto hao, Joyce Mrema, alisema watoto wake walianza kuacha kula vyakula vya kawaida hasa vigumu kama mkate, ugali na wali, walipofikisha umri wa miaka mitatu hadi sasa.

Kwa mujibu wa mama huyo, watoto hao kwa sasa wanakula magodoro kwa kujificha, huku akieleza kuwa ana hofu huenda tatizo hilo linaweza likawasababishia kuziba kwa utumbo unaoruhusu chakula kufika tumboni.

"Nilishawahi kuwapeleka hospitali ndogo ya Levolosi, nikaambiwa wamekosa madini fulani. Nikashauriwa niende nyumba ya Mungu, Mwanga (mkoani Kilimanjaro) nikachukue dagaa niwachemshe na kumekucha niwape wanywe na kuwachemshia 'corn flower' za kijani. Najaribu wapi wanakula magodoro tu," alibainisha.

Alisema magodoro ndani yanaisha hali inayomlazimu kwa sasa kuwafungia nje anapokuwa ametoka au anapofanya shughuli zake nje ili kuwadhibiti.



Watoto mapacha wanaoishi kwa kula magodoro wakiwa na mama yao, Joyce Mrema, nyumbani kwao, Mtaa wa Kanisani, Kata ya Sokoine One, jijini Arusha. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

Pia alisema hata akichemsha maziwa au mayai hawali. "Wanakuangalia tu kama unafanya shughuli, wanaenda chooni kumwaga," alisema.

"Kuna siku niliwakagua mabegi ya shule nikakuta chakula kimewekwa huko kimekauka nikajua kumbe hawali chakula. Wakipewa wanaficha hadi kinaweka ukungu, kazi ni kula magodoro na nikiangalia matapishi nakuta vipande vya godoro," alisema.

Alisema hata wanapokwenda shuleni wanaiba vifutio vya walimu vya magodoro wanaleta nyumbani wanakula kwa siri.

"Kuna wakati niliwahi pata kesi kwa jirani yangu mmoja waliende kucheza na wenzao wameingia ndani wakaanza kuchokonoa mito ya makochi na kula godoro. Lakini kwa mama yangu huko Ngulelo hapa Arusha, ambaye ni bibi yao, walikwenda huko kuna wakati nako nikaambiwa wakila wanatapika na walipoangalia waliona vipande vya godoro vingi," alifafanua.

Alisema kutokana na tatizo hilo kwa sasa hana uwezo wa kuwapeleka hospitali kubwa na kazi yake ni ya kufua nguo za watu kwenye nyumba tofauti tofauti.

"Kazi hii napata kipato kidogo na nilianza mwaka 2013 hawa watoto wakiwa na mwaka mmoja na miezi mitatu baada ya baba yao kunikimbia alipokopa fedha kwa watu," alisema.

Alisema baada ya mume wake kukimbia deni hilo na mkopaji alifungua kesi mahakamani anadai Sh. milioni 33, akishinda kesi atauza nyumba yake na kwamba katika kesi hiyo, anasaidiwa na wanasheria wa haki za binadamu.

Kwa mujibu wa mama huyo, katika suala hilo la mkopo, mume wake hakumshirikisha wakati akikopa Sh. milioni tatu lakini kutokana na kukaa nao kwa muda mrefu, deni limeongezeka mpaka kufikia Sh. milioni 33 ambazo hana.

"Lakini sielewi kwa nini watoto wangu wanakula magodoro, sababu hata nikiwa mjamzito nilikuwa napenda kula machungwa sana, kitu ambacho ni tunda hakina madhara," alisema.

Mrema alisema ameshawapeleka watoto hao kwenye maombi sehemu tofauti tofauti wakaombewa lakini bado wameendelea kula magodoro.

"...Kweli naomba msaada Watanzania wanisaidie niwapeleke hospitali kubwa labda watapata matibabu."

Kwa upande wao watoto hao, walisema wanatamani kuacha kula magodoro na hawapendi kufanya hivyo, lakini wanajikuta wanapata hamu ya kula magodoro kila wakati kuliko chakula chochote. Walisema walishawahi kuwaza kuacha lakini hawajui kwa nini hawawezi kuacha. Wanaomba Watanzania wawasaidie wakatibiwe, ili waache kula magodoro waishi kama watoto wenzao kwa kula chakula cha kawaida.

Watoto hao walisema licha ya mama yao kuwazuia kula magodoro, kila siku wao wanakula kwa kuwa hawawezi kupitisha siku bila kuyala.

Kwa mtu yoyote aliyeguswa kusaidia watoto hao, wakapate matibabu watumie fedha zao kupitia namba ya mama wa watoto hao **0763876313** jina Joyce Mrema.


DANISH REFUGEE COUNCIL

## TANGAZO LA ZABUNI

**SHIRIKA LA DANISH REFUGEE COUNCIL LINATARAJIA KUINGIA MKATABA WA UNUNUZI WA VIFAA VYA KUTENGENEZEA MKAA MBADALA.**

SHIRIKA LA DANISH REFUGEE COUNCIL LILILOPO KIBONDO LINAWAARIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISH REFUGEE COUNCIL KIBONDO KUANZIA TAREHE 20.05.2022 HADI TAREHE 2.06.2022 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA **+255624 399 911** au BARUA PEPE **josphat.mwangi@drc.ngo**

ZABUNI ZITAFUNGULIWA TAREHE **3.06.2022 SAA 4:00 ASUBUHI** OFISI ZA DANISH REFUGEE COUNCIL KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISH RFUGEE COUNCIL PEKEE KUTOKANA NA MLIPUKO WA UGONJWA WA UVIKO-19. HIVYO WAWAKILISHI WA KAMPUNI HAWATORUHUSIWA KUSHIRIKI UFUNGUZI.

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@drc.ngo AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.**


# Vipaumbele vya Wizara ya Ulinzi 2022/23

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WIZARA ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeainisha vipaumbele vyake ambavyo imepanga kuvitekeleza katika mwaka wa fedha 2022/23 na kuomba kuidhinishiwa Sh. trilioni 2.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo jana bungeni ambayo ilipitishwa, Waziri wake, Stergomena Tax, alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kuendeleza jitihada za utatuzi wa matatizo ya mipaka na nchi jirani.

Alitaja vingine ni kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na raia.

"Vingine ni kuendelea kulipa malipo na posho kwa wanajeshi, mashamba na stahili kwa watumishi wa umma. Kujenga uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuboresha miundombinu ili iweze kuchukua vijana wengi zaidi na kutoa mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, Umoja wa Taifa na stadi za kazi kwa vijana," alisema.

Vipaumbele vingine alivitaja ni kuendelea kujenga uwezo JKT ili kuiwezesha kujitosheleza kwa chakula kwa vijana wanaojiunga na mafunzo.

"Kuendelea kuimarisha na kuratibu mafunzo ya Jeshi la Akiba kwa kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuhusu masuala ya ulinzi, uzalendo wa kitaifa, usalama na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi wa nchi," alisema.

Waziri huyo alitaja vingine ni kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya za Kikanda na nchi mbalimbali katika nyanja za kijeshi na kiulinzi.

Pia alisema kuendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura itakapohitajika.

Kadhalika alisema kuendelea kutatua migogoro ya ardhi kwa kupima mipaka ya maeneo ya jeshi, kufanya uthamini na kulipa fidia ya ardhi iliyotwaliwa kutoka kwa wananchi kwa matumizi ya jeshi.

Pia alisema wizara kupitia Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), imeendelea kupanga, kuratibu na kusimamia mafunzo ya maofisa na askari nje ya nchi ambapo hadi kufikia Aprili 30, mwaka huu, waliopatiwa ni 490.

Alisema mafunzo kwa Jeshi la Akiba kwa wananchi katika ngazi ya awali katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili mwaka huu waliopatiwa na kuhitimu ni 12,510 na kati yao wanawake ni 1,760.

"Mafunzo kwa vijana kwenye kambi mbalimbali kupitia operesheni ya Samia Suluhu jumla ya vijana 25,503 kwa mujibu wa sheria wamepatiwa mafunzo na kati yao wanawake ni 5,959," alisema.

Alisema kwa vijana wa kujitolea waliopatiwa ni 11,739 na kati yao wanawake ni 3,574.

"Shirika la mizinga limepokea Sh. bilioni 5.465 kati ya Sh. bilioni 5.5 sawa na asilimia 99.37 ikiwa ni sehemu ya fedha za maendeleo zilizopokelewa na wizara na kuweza kutekeleza shughuli za maendeleo ikiwamo ununuzi na ukarabati wa mitambo, uzalishaji wa zao la msingi, vipuri na zana.

# MATANGAZO


TEMBO NICKEL

# VACANCY

## LEGAL & COMPLIANCE SPECIALIST

**Position Summary:**
Tembo Nickel is seeking to recruit a **Legal & Compliance Specialist** to join the Tembo Nickel Project Team. This role is based in Dar es Salaam, reporting to the Head of Human Resources

**Principal Accountabilities**
1. To lead and manage all legal and compliance issues for Tembo Nickel
2. To provide legal advice across Tembo Nickel to all levels of managment on a wide variety of issues and cases.
3. To perform all legal administrative duties including BRELA corporate filings, business license renewals, tax clearance certificates in addition to handling regulatory matters.
4. To keep up to date with and scrutinise new legislation, statutory instruments, policies, circulars, case law and guidance, evaluate their effect and give timely and proactive advice on them to the management of Tembo Nickel.
5. To be responsible for effective time recording of matters and performance reports, ensure appropriate allocation of resources and effective monitoring, and to support the team in performing their roles.
6. To undertake and oversee cost recovery on appropriate work ,utilising time recording information to ensure that Tembo Nickel interests are protected, and to undertake appropriate cost control measures on individual matters.
7. To contribute positively to the performance of the governance team.
8. To establish effective working relationships and ensure that effective communication and engagement takes place with management and staff,
9. To support, contribute and comply with quality and governance procedures as directed by management.
10. To personally provide legal advice on various matters including but not limited to Labor, Commercial/Procurement, Planning/Property, Civil and Criminal Litigation.
11. To manage the legal service workload to ensure performance management targets are met.
12. To support Tembo Nickel in ensuring compliance with its governance responsibilites including the preparation of documents for Board meetings and Annual General Meetings and to attend such meetings as and when required. To advise on corporate, legal, and probity issues and to promote best practice and good order in such meetings.
13. To lead Tembo Nickel legal services and to provide high quality professional advice across the company, which is both proactive and responsive to Tembo Nickel requirements.

**Experience and Qualifications**
- Bachelor's degree in law
- Must be a registered advocate
- Minimum of Five (5) years working experience in a similar role in a reputable organization/firm
- Knowledge of key legislation and issues relating to mining will be an added advantage
- Evidence of working effectively within a multicultural environment, providing clear advice and guidance on complex matters should they arise.

Tembo Nickel offers a competitive remuneration package and ONLY shortlisted candidates will be contacted.

**How to Apply**
Applicants are invited to send their resume **indicating the role title in the subject via the email** **jobs@tembonickel.com**

**Application closing date is 3rd June,2022**

**Note:** Tembo Nickel is an equal opportunity employer and all appointments are based on merit. The company does not charge candidates any fees in the recruitment process

216864301



TOL Gases Limited
We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

# TOL GASES LIMITED
# "WE DELIVER"

PLOT 4B NYERERE ROAD, P.O.BOX 911 DSM, TEMEKE DISTRICT, DAR ES SALAM, TANZANIA

## BID FOR SALES OF USED VEHICLES, ENGINE & GENERATOS

| ITEM NO | VEHICLE REG NO | MAKE | LOCATED | STATUS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | T836 CUB | TOYOTA CARINA | DSM | RUNNING |
| 2 | T384 BYL | NISSAN NAVARA | DSM | NOT RUNNING |
| 3 | T628 BYL | NISSAN NAVARA | DSM | NOT RUNNING |
| 4 | T588 BYL | NISSAN NAVARA | DSM | RUNNING |
| 5 | T178 CZS | TOYOTA LANDCRUISER | DSM | RUNNING |
| 6 | T206 DJK | SCANIA 124 TRACTOR | DSM | RUNNING |
| 7 | T396 ATS | SCANIA R114 | DSM | RUNNING |
| 8 | T451 DLD | IVECO TRACTOR | DSM | RUNNING |
| 9 | T619 BYL | SCANIA P380 | DSM | NOT RUNNING |
| 10 | T308 DLH | IVECO TRACTOR | DSM | NOT RUNNING |
| 11 | USED ENGINE | SCANIA R440 NW081127 | DSM | IMPORTED FROM ENGLAND |
| 12 | USED ENGINE | NISSAN NAVARA – EN.AC46500# | DSM | IMPORTED FROM ENGLAND |
| 13 | USED GENERATOR | JOHN DEERE, 250KVA- with separated alternator and housing | DSM | NOT WORKING |
| 14 | USED GENERATOR | FIAT, 80KVA – complete with alternator | DSM | NOT WORKING |
| 15 | USED GENERATOR | FIAT, 125KVA- complete with alternator | DSM | NOT WORKING |

The vehicles and generators may be viewed by APPOINTMENT at TOL GASES LIMITED, Nyerere Road, Temeke District, Dar es salaam, Tanzania during weekdays from 9.00 to 16.00 hours and Saturday from 9:00 to 12:30 by contacting mobile number 0685 750 219 (Rajabu Kiweku)

**TERMS AND CONDITIONS**
1. All bids should be submitted in a sealed envelope, addressed to the Managing Director (MD) P.O.BOx 911 DSM and clearly marked "Sale of Vehicles" ,"Sale of Generator" or "Sale of Engine" should be deposited in the Tender Box located at the MD'S office, at TOL Gases Ltd in DSM not later than Friday 17th June 2022 at 16:00hrs (local time)
2. Nonrefundable tender fees of Tzs 20,000/= should be paid direct to our company cashier or Deposited in our CRDB Account No. 01J1005018900 (Tol Gases Ltd) and the acknowledged payment receipt should be attached to the tender bids.
3. Offers received after the specified closing date and time will not be considered.
4. The successful bidder shall be required to effect full payment of the bid.
5. The Tol Gases Ltd, reserves the right to accept or reject any offer and to cancel the above exercise at any time prior to award without thereby incurring any liability to affected bidder(s).
6. All quotes should be inclusive of VAT-18%.
7. The sold vehicle will only be allowed to leave the company yard after the transfer of ownership process is completed.
8. The Buyer must provide his/her details including TIN and NIDA ID
9. It is understood by the Buyer that the vehicle, engine, or generator is sold as seen, tested, and where it is (Tol Gases Ltd yard) and approved without any guarantee, either explicit or implied, after sale. **"The Vehicle, engine or Generator is sold as seen condition"**

**Closing Date: Friday, 17th June 2022.**

216863802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli ya Samia kwa wabunge ni sahihi

**JUMATANO,** Rais Samia Suluhu Hassan, aliwashangaa wabunge wanaorodhesha matatizo ya maeneo yao, huku akiwataka wawajibike kuepuka kuwa walalamikaji kwa kuhamasisha wadau kuchangia shughuli za maendeleo.

Aidha, aliwataka kuhimiza wafanyabiashara kulipa kodi, ili kuongeza mapato ya serikali badala ya kudai maendeleo katika maeneo yao, kwa kuwa wana nafasi kubwa kuhakikisha wanasimamia na kuhimiza ulipaji kodi.

Alisema kuwa serikali haina muujiza wa kupata mapato bila kukusanya kodi kutoka kwa wananchi, na kwamba wabunge wana nafasi kubwa katika jambo hilo.

Pia, alisema wabunge wanaolalamika kwenye maeneo yao kuna wafanyabiashara wenye maduka makubwa na madogo wanaopaswa kuhamasishwa kulipa kodi ili fedha ipatikane.

Alichokisema Rais Samia ndicho kinaonekana siyo kwa wabunge tu bali hata viongozi wa serikali, kasumba ambayo imekuwa kawaida kwa wananchi kiasi cha kuamini kuwa matatizo yao yatatatuliwa na serikali pekee.

Ndiyo maana Rais anavyofanya ziara kwenye eneo fulani atapokelewa na mabango yenye orodha ya matatizo ya wananchi, mbunge naye akipewa nafasi kuzungumza jukwani ataorodhesha mengi anayotaka serikali iyafanyie kazi, akija mkuu wa wilaya, mkoa na wengine wataweka orodha kila mmoja akiomba fedha kutoka kapu kuu.

Kutokana na fikra hizo imepelekea kwamba wananchi wanashindwa kutatua changamoto za maeneo yao zinazoweza kutatuliwa kwa kuwa wanaisubiri serikali iwafanyie kazi kwa kuwa wameaminishwa kuwa ndiyo wenye wajibu huo.

Mara kadhaa wabunge wamekuwa wakilalamika au wakati mwingine kuieleza serikali bila kutoa ushauri wa nini kifanyike, jambo ambalo linakuwa siyo msaada bali mtu kapaza sauti tu.

Ni lazima kila mmoja kwa nafasi yake kuisaidia serikali kutekeleza majukumu yake, kwamba wananchi wote tulipe kodi kwa usahihi na kuhamasisha wananchi kufanyakazi za kutatua changamoto za maeneo yao bila kusubiri serikali pekee.

Tunaona ni muhimu viongozi wakawajenga wananchi katika kufanya kazi za kijamii na siyo kusubiri kufanyiwa, enzi za utawala wa Mwalimu Julius Nyerere, Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete wananchi walifanyakazi za kuchimba barabara, kujenga shule kwa kutoa nguvu kazi kuondoa dhana ya mali ya umma.

Zipo barabara zimejengwa kwa nguvu ya wananchi kutokana na viongozi kuwa mstari wa mbele kuwahamasisha na kushiriki kwa vitendo kufanya kazi hizo, kwamba hawatasubiri kiongozi aje ndiyo waorodheshe matatizo.

Tunajua yapo maendeleo ambayo lazima yagharamiwe na serikali, lakini sasa tunapaswa kuhimiza moyo wa kujitolea, kwamba kusiwe na kukatisha tamaa kwamba kuna wanaopata fedha wakati wengine wanavuja jasho.


Awamu ya kwanza ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wananchi walikuwa wanaibua vipaumbele kwenye eneo lao, kisha inafadhiliwa kwa asilimia 80 huku nguvu kazi ikitolewa na wananchi kwa kufyatua tofali, kuchimba msingi, kuchimba barabara na nyingine.

Kwa mazingira yetu bado hatujafikia hatua ya serikali kufadhili kila mradi kutokana na fedha zilizoko, bali wadau wa maendeleo wa ndani na nje wanashiriki ambao ili kuwatambua ni lazima kuwahamasisha kuchangia shughuli za maendeleo.

Kwenye kila eneo kuna viongozi wa kuchaguliwa kuanzia mwenyekiti wa kitongoji/mtaa, kijiji, Diwani, Mbunge na Rais, wote hawa wanawakilisha wananchi katika kuendesha serikali.

Ikiwa kama mwenyekiti wa mtaa atapeleka malalamiko kwa aliyejuu yake, naye akayasogeza mbele maana yake ni kutengeneza mlolongo wa malalamiko bila kuona suluhisho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Halfani Chusi

# Jamani, hakuna uchuro aina yoyote tunapoandikia warithi wosia wetu

**SULUHU** ya kumaliza migogoro ya mirathi katika familia, ni kuandika wosia kama watu wakijenga utamaduni wa kuandika wosia pasi na shaka migogoro ya mirathi haikuwapo, wala kuchomana visu kwa kugombania mali za urithi.

Tatizo ni kwamba, watu wengi wanaogopa kuandika wosia kwa imani potofu kwamba mtu anajichulia kifo kwa lugha nyepesi wanaita 'uchuro,' kitu ambacho sio sawa na kufa kupo tu, kikubwa ni kuwatengenezea mazingira mazuri watoto wako kabla ya kufa, ili mali zilizopo zisiwagawe na kuwatengenezea matabaka.

Pia, wapo wanaoamini maskini hatakiwi kuandika wosia, kwa kuwa hana mali kama ilivyo kwa tajiri. Lakini, kitu pekee cha kusema hapa, ni bora ukaandike wosia hata kwa kidogo ulicho nacho, kuliko kuingiza hizo imani kwa kuwa baada ya hapo utaiachia familia migogoro isiyokwisha.

Utafiti kuhusu wosia, umebaini theluthi mbili ya watu hawana uelewa wowote kuhusiana na dhana hiyo na umuhimu wa uwekaji wosia huku baadhi yao wakiamini ni uchuro na kwamba suala hilo ni la matajiri.

Ripoti ya Haki za Binadamu 2021, iliyozinduliwa hivi karibuni mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga, iliyojikita katika maeneo matatu, ikiwamo haki za binadamu, kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni na haki jumuishi inafafanua.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kuhusu wosia na kugawanywa katika makundi sita, ilibaini asilimia 72 walisema hawako tayari sababu bado vijana, asilimia 63 walisema hapana wakidai ni uchuro na asilimia 76 wakidai hawawezi kuandaa sababu hawana mali za kutosha.

Aidha, asilimia 15 walisema wapo tayari kuandaa wosia kwa mdomo na si maandishi, huku asilimia 44 wakisema hawana uelewa kuhusu suala hilo.

Ni mada na dhana inayoniinua kwenye kiti na kuzuru mtaani kusaka ukweli ulikosimamia. Hapo ndipo naonana na Jacob Kilamba, kutoka Iringa anayetoa mtazamo wake kuhusu kuandika wosia. Hapo nabaini kuwa si kwamba watu wengine hawataki kuandika wosia, bali wengine pia hawana uelewa wa kutosha hata juu ya kuandika wosia, pengine hawatambui hata kidogo nini maana ya wosia. "Watu hawataki kuandika wosia wakiamni ni kujichuria kifo. Wengine wanaamini wosia ni kwa ajili ya walio na mali nyingi," anavyonijibu Jacob.

"Suala la kuandika wosia ni la watu wa mjini, kwa sababu wao ndio wasomi. Katika jamii yetu hapa kuandika wosia kunamaanisha kuanzisha migogoro ya kifamilia," naye akajibu mkazi wa mkoani Iringa, baada ya kuhojiwa na Nipashe.

Hata mwanahabari ninapopiga hodi hadi kijiji cha Mgowelo hukohuko Iringa kudodosa juu ya wosia na kumpata Limo Kilamba, anayetoa mtazamo wake kuhusu kuandika wosia.

Ananijibu: "Kuna wazee ambao wanaishi kwa hofu ya watoto wao wenyewe, wakijua kwamba wana uwezekano mkubwa wa kupigwa na watoto wanagundua kuwa kuna wosia.

"Baadhi ya watu huandika wosia wakiwa wagonjwa sana na kufariki muda mfupi baadaye. Kama matokeo, wosia hupotea au katika hali mbaya zaidi ya asili itafichwa na baadhi ya wanafamilia," anasema.

Rai yangu kwa serikali kufungua darasa la kuelimisha jamii juu ya masuala ya kuandika wosia, ili kupunguza mrundikano wa kesi nyingi mahakamani, ambazo kila uchwao utasikia tunagombania mali za urithi.

Vivyo hivyo, ukidodosa tatizo unagundua aliyekufa hakuandika wosia juu ya mali zake, ili iwe rahisi katika kugawanya mali na watu wakielimika katika hilo itasaidia kupunguza vifo vya ndugu, ambavyo vimekuwa vikitokea kwa ajili ya kugombania mirathi.

**Mwandishi anapatikana kaa simu: 0787879707**

# Serikali yatoa kipaumbele ajira kwa wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imetoa kipaumbele kikubwa cha ajira kwa watu wenye ulemavu na kuwataka wajitokeze kwa wingi kuomba nafasi hizo yanapotolewa matangazo.

Aliyasema hayo jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Stella Ikupa, kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

Mbunge huyo alitaka serikali inapotangaza nafasi za ajira, itenge asilimia fulani kwa ajili ya wenye ulemavu tofauti na utaratibu uliopo sasa.

Majaliwa alisema serikali imeweka utaratibu maalumu wa uendeshaji wa michakato ya ajira katika Sekretarieti ya Ajira na kutoa upendeleo kwa watu wenye ulemavu pale zinapotangazwa ajira.

"Hata katika teuzi mbalimbali anazozifanya Mheshimiwa Rais Samia ametoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu. Hata hivyo, watu wenye ulemavu wanapata fursa ya kwanza kwenye usaili wa ajira mbalimbali."

Wakati huo huo, Waziri Mkuu asema katika kuhakikisha Bandari za Mtwara na Tanga zinatumika ipasavyo, serikali imeamua kutoa punguzo la asilimia 30 ya tozo katika gharama za kuhudumia shehena na meli kama sehemu ya mikakati ya kimasoko na kuvutia wateja kutumia bandari hizo.

Alitoa kauli hiyo wakati akijibu swali la Mbunge wa Nanyamba, Abdallah Chikota aliyetaka kujua serikali ina mikakati gani wa kuwavutia wafanyabiashara wa Malawi, Zambia na Congo, kutumia Bandari ya Mtwara na nchi nyingine ikiwamo Sudan Kusini na Uganda kutumia Bandari ya Tanga.

"Ni kweli kwamba serikali kupitia Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imetenga fedha kwa ajili ya maboresho ya bandari zetu zote nchini zilizoko ukanda wa bahari kuu na pia kwenye maziwa makuu kwa ajili ya kuimarisha miundombinu mbalimbali."

"Tumeongeza vifaa vinavyoweza kupakia na kupakua mizigo kwa muda mfupi, pia tumepunguza tozo katika Bandari za Tanga na Mtwara ili wateja wanaoleta mizigo katika bandari hizo na kuwahakikishia wateja upatikanaji wa huduma kwa muda mfupi zaidi."

Majaliwa aliwakaribisha wafanyabiashara wa mafuta kutumia bandari hizo kwa kuwa licha ya kupunguza tozo, pia serikali imefunga mita za kisasa za kupakua na kupakia mafuta ili kurahisisha upakuaji na upakiaji wa shehena hiyo na wamejenga matangi ya kutosha.

Alisema Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), inatumia balozi zilizoko nchini kuhamasisha wafanyabiashara wa huko kutumia Bandari ya Tanzania na imefungua ofisi katika nchi za Congo, Malawi na Zambia ili wateja wanaohitaji huduma kupitia bandari hiyo wapate mawasiliano wakiwa katika nchi zao bila ya kulazimika kuja Tanzania. Pia, amewahakikishia wafanyabiashara hao usalama wao na mizigo yao na kuwataka waendelee kutumia vyema bandari hizo.

## Ripoti ya mawaziri migogoro ardhi kuwasilishwa bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema ripoti ya kamati inayoongozwa na mawaziri wanane kushughulikia migogoro ya ardhi nchini, itawasilisha bungeni mara tu itakapomaliza kazi yake.

Majaliwa alieleza hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Morogoro Mjini (CCM), Abdulaziz Abood, aliyehoji kuhusu upimaji wa ardhi kwenye maeneo yenye migogoro na yanayotajwa kuwa ni vyanzo vya maji ambako baadhi ya wananchi wako mbali lakini wanatakiwa kubomolewa.

"Jambo hili limekuwa likitoa taharuki kubwa kwa baadhi ya wananchi kwenye maeneo haya naomba serikali kutoa tamko la kuwaondolea hofu wananchi," alisema.

Akijibu swali hilo, Majaliwa alisema kamati hiyo inakaribia kumaliza kazi ya kuitambua migogoro hiyo na ripoti yake itawasilishwa bungeni kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

"Timu ya mawaziri wanane imeendelea kufanya kazi kwa maeneo yote yenye migogoro ilianza kufanya kazi mwaka 2019 na tayari ilishawasilisha taarifa bungeni kuhusu vijiji vilivyopitiwa, migogoro mingi inamalizwa na ngazi ya viongozi ya vijiji, kati, wilaya na mkoa."

"Lakini, matatizo makubwa ndiyo yanashughulikiwa na timu ya mawaziri wanane ambayo inatarajia kukamilisha kazi yake muda mchache na kuwasilisha taarifa bungeni," alisema.


bgtl

**BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **NMB BANK PLC** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zilizodhamini mkopo wake kwa MNADA WA HADHARA.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana zilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAWI |
|---|---|---|---|
| 1. | SPRINT CORPORATE LIMITED/BEATUS GODBET RUGE | Kiwanja kilichopo maeneo ya Kulangwa Manispaa ya **Kinondoni,**Dar es salaam kwa jina la **Beatus Godbet Ruge** | TEGETA |
| 2 | JOYCE GIDIONI KWAYU | Nyumba ya makazi iliyopo Vianzi, Wilaya ya Mkuranga,Pwani. | KARIAKOO |
| 3 | NASSIR FOCUS NDESSI/THERESIA ERICK SHAYO | Nyumba yenye leseni ya makazi na. TMK041580 iliyopo Mianzini Charambe, Manispaa ya Temeke kwa jina la Theresia Erick Shayo | KARIAKOO |
| 4 | YUSUPH MBOETO | Nyumba ya makazi iliyopo mabibo sahara yenye leseni ya makazi KND/MBB/MBO16/114 Manispaa ya ubungo | ILALA |
| 5 | ZAHARA HUSSEIN | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye Kiwanja chenye **Leseni** ya makazi maeneo ya **Mangaya Mbagala TMK/MBGL/MAN11/269A Manispaa** ya **Temeke** | MBAGALA |
| 6 | BAKARI SELEMANI BANYANGA | Nyumba ya makazi yenye Hati ya mauziano iliyopo maeneo ya Mbagala Kilungule | KARIAKOO |
| 7 | BENSON NAHUM KABERE | 1) Nyumba ya makazi yenye kipande cha ardhi na.TMK/MBGL/KZG5/299 yenye leseni no TMK032102 iliyopo kizinga manispaa ya temeke<br>2) Nyumba ya makazi yenye kiwanja no 28&29 kitalu H leseni no.139102 na no.551610 iliyopo chamazi manispaa ya ilala | KARIAKOO |
| 8 | YUSRA ALLY RAMBO | Nyumba ya makazi iliopo kwenye kiwanja kilichopo Mtoni relini. | KARIAKOO |
| 9 | HAJI ISMAIL | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye Kiwanja chenye Hati ya mauziano maeneo ya Ponde Twangoma Manispaa ya Temeke. | ILALA |
| 10 | TANTON IMAGING TECHNOLOGY/KUMBUKA DEUS NTEJA | Nyumba ambayo haijakamilika iliyopo kigogo kati yenye leseni ya makazi KDD/KGG/KST11/82 | ILALA |
| 11 | ERICK AMANI SWAY | i. Nyumba ya makazi yenye kipande cha ardhi na.TMK/CHB/KIM2/53 iliyopo charambe mtaa wa kilungule,manispaa ya Temeke yenye Leseni na.TMK035418 kwa jina la Nuhu Ismail Kaitila<br>ii.. Nyumba ya makazi yenye kipande cha ardhi na.TMK/MBGL/MOR2/410 iliyopo Mbagala mtaa wa Moringe, manispaa ya Temeke yenye Leseni na.TMK041863 kwa jina la Juma Hamisi Kitogo | B/CENTRE. |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/ mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537
Email: info@bestgoup.co.tz

AU

Mkurugenzi Mtendaji
NMB Bank PLC,
Ohio Street / Ali Hassan Mwinyi Road,
P.O. BOX 9213,
DAR ES SALAAM
Telephone: +255 22 2322550
email: Benedicto.Baragomwa@nmbbank.co.tz



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

**TAARIFA KWA WALIOKUWA WAFANYAKAZI WA MGODI WA DHAHABU WA BULYANHULU**

Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu (OWM KVAU) kwa nyakati tofauti imekuwa ikipokea malalamiko ya waliokuwa wafanyakazi wa Mgodi ya Bulyanhulu dhidi ya Mwajiri wao kuhusu kutopimwa afya, kutokupatiwa matibabu na kutokulipwa fidia.

Serikali kupitia Wizara yenye dhamana na masuala ya Kazi na Ajira imekuwa ikishughulikia malalamiko hayo kupitia Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA), Turne ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) na Idara ya Kazi.

Kwa mara ya mwisho mnamo mwaka 2021 Wizara yenye dhamana ilipokea, kuchambua na kutolea maamuzi malalamiko 150 ya waliyokuwa wafanyakazi Bulyanhulu. Hata hivyo waliokuwa wafanyakazi wa kampuni hiyo wameendelea kuwasilisha malalamiko katika mamlaka mbalimbali za Serikali.

Ofisi imepokea malalamiko kadhaa ambayo yataanza kuchambuliwa iii kuyatolea maamuzi. Hivyo, ninapenda kuwataarifu wale wote ambao malalamiko yao hayajawahi kuwasilishwa na kutolewa maamuzi na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kuwasilisha malalamiko yao iii nayo yafanyiwe kazi kwa pamoja. Malalamiko hayo yawasilishwe mapema iwezekanavyo kabla ya tarehe **8 Juni, 2022** yakionesha Jina, Namba ya ajira, Mahali anapoishi na Namba ya simu ya mlalamikaji. Malalamiko hayo yawasilishwe kupitia anwani ifuatayo:-

**Katibu Mkuu,**
**Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,**
**S. L. P. 2890,**
**Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma.**

**Au**
**Barua pepe: ps@kazi.go.tz**

**IMETOLEWA NA KATIBU MKUU**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

# NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **MASE INTERNATIONAL LIMITED, JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER, JUCACO AUCTION MART na JADA INVESTMENT LIMITED** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD,** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | JADA INVESTMENT LIMITED | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | Paul Nyabiginga Wangubo | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kitunda-Dar es Salaam |
| 2 | Lucy C Mwakajinga | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mtambani- Vingunguti Dar es Salaam |
| 3 | Nobert L Kwiyaka | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Chamazi-Dovya- Dar es Salaam |
| 4 | Chelile Fimbo Kapini | Nyumba yenye mkataba wa mauziano Mali ya Shija Italange Mahona | Mbagala Kuu Mission-Dar es Salaam |
| 5 | Mariam Meck Makura | Nyumba yenye mkataba wa mauziano mali ya Anthony Mugambo Makuke | Saranga-Kimara B - Dar es Salaam |
| | JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER | | |
| 6 | Alfred James Mhalu | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Katoro Center-Geita |
| 7 | Elias Benjamini | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Bulengahasi Katoro-Geita |
| 8 | Paskali C Lugedenga | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mtunduni Katoro-Geita |
| 9 | Charles Mubarikiwa Gatuja | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mtaa Wa 14 Kambarage-Geita |
| 10 | Kabalo Silugwaye Ndone | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kabuyombo Kasamwa-Geita |
| | MASE INTERNATIONAL LIMITED | | |
| 11 | Angel J.Tarimo | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano mali ya Anna Peter Silvanus | Nyegezi-Majengo-Mwanza |
| 12 | Emmanuel S.Nchalla | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kisiwani-Mhandu-Mwanza |
| 13 | Mwita B.Saguti | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kashishi-Nyamhogoro-Mwanza |
| 14 | Lameck M.Nkanda | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Nyabusalu-Kiseke-Mwanza |
| 15 | Ayoub Wilson Lusiji | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Busekwa-Kiseke-Mwanza |
| 16 | Daniel Y Kubebeka | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Isangijo-Kisesa- Mwanza |
| 17 | Phibe K.Agwanda | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kilimahewa-Mwanza |
| | JUCACO AUCTION MART | | |
| 18 | Ackim Jamlon Tweve | Nyumba yenye Leseni ya Makazi | Minazi Mirefu-Kiwalani-Dar es Salaam |
| 19 | Samson.M. Buswelu | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Gogo-Kimwani-Chanika-Dar es Salaam |
| 20 | Rajabu Hamisi Mkonge | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Kisemvule-Mkuranga- Dar es Salaam |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atakayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mase International Limited**
**S.L.P Mwanza**
**Namba Za simu: 0710885084/0714208208**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji.**
**Jucaco Auction Mart**
**S.L.P Dar es Salaam**
**NAMBA ZA SIMU: 0712552699**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**

**Jada Investment Limited**
**S.L.P 4110 Dar es Salaam**
**NAMBA ZA SIMU: 0788493699**

**Na**

**Josina Company Limited & Auctioneer**
**S.L.P Mwanza**
**NAMBA ZA SIMU: 0713203040/0789203040**

**NA**

**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**DAR ES SALAAM**
**NAMBA ZA SIMU: 0768790399/0754774949**

# NMB kufadhili wanafunzi wa sekondari, elimu ya juu

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya NMB Foundation imetangaza kuanza rasmi utaratibu wa kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kidato cha tano, sita na elimu ya juu baada ya programu hiyo kuzinduliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa mwishoni mwa mwaka jana.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Bodi ya NMB Foundation, Ruth Zaipuna, alisema wameanza kupokea maombi kupitia matawi yote ya benki hiyo yaliyoko nchi nzima na tovuti ya NMB Foundation.

"Kwa kuanzia tutatoa ufadhili kwa wanafunzi 200, ambapo 150 watakuwa wa kidato cha tano na sita, wanafunzi 50 watakuwa wa elimu ya juu. Ufadhili utalipia gharama zote za masomo ikiwamo ada, fedha za kujikimu, vifaa na mahitaji mengine yatakayotajwa kwenye fomu ya kujiunga na shule au chuo," alisema Ruth.

Alifafanua kuwa kwa wanafunzi wa sekondari watakaopata ufadhili watalipiwa ada, nauli, vifaa vya kujifunzia, fedha za kujikimu, bima ya afya na mahitaji mengine watakayotakiwa kutoka shule. Kwa upande wa elimu ya juu, wanafunzi watalipwa ada, fedha za kujikimu, fedha za mafunzo kwa vitendo, Laptop na gharama nyingine watakazotakiwa kwenye fomu ya kujiunga na chuo.

Aidha, Zaipuna alisema wamejipanga kuweka masomo ya vipaumbele kwa wanafunzi watakaopata fursa ya udhamini. Lengo ni kuhakikisha wanashiriki mabadiliko ya kijamii na kiuchumi kupitia malezi na mafunzo watakayopata wanafunzi hao.

"Tutaangalia kwa kina masomo ya takwimu na mahesabu, biashara na uchumi, teknolojia ya mawasiliano ya umma, uhandisi, mafuta na gesi pamoja na sayansi na teknolojia," alibainisha Zaipuna na kuongeza:

"Nina imani kupitia programu hii tutaibua vipaji na tutatimiza ndoto za vijana. Kadiri tutakavyoendelea idadi ya wanafunzi watakaonufaika itaongezeka kulingana na mahitaji ambapo tutapanua wigo wa wadau wengine watakaotaka kushirikiana nasi kwenye jambo hili muhimu kwa maendeleo ya nchi."

Katika hatua nyingine, Ruth alisema NMB Foundation itahakikisha watu wakatohusika kukusanya na kupitisha wanafunzi wanaofaa kwa kupewa ufadhili watakuwa makini kutimiza vigezo, ambapo kwa wale watakaokwenda kinyume na utaratibu watachukuliwa hatua za kinidhamu. "Tunataka kulifanya zoezi hili liwe na uwazi na ukweli, ndio maana tumesema tutawashirikisha hata viongozi wa serikali za mitaa kuanzia kata hadi mitaa, lengo ni kuhakikisha wanufaika watakaopatikana ni kweli wana vigezo vinavyohitajika," alisisitiza Zaipuna.

# Mawaziri wazungumza na waathirika wa 'panya road'

**Na Sabato Kasika**

WANANCHI wametakiwa kushirikiana na serikali bega kwa bega kwa kutoa taarifa za uhalifu na viashiria vyake katika maeneo yao, ili kusaidia kukomesha vitendo hivyo ndani ya jamii.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na mawaziri Dk. Dorothy Gwajima wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni. Mawaziri hayo walipotembelea kata za Chanika, Zingiziwa na Buza kuzungumza na waathirika waliovamiwa hivi karibuni na vijana wadogo 'panya road', wenye silaha yakiwamo mapanga kuwakata na kuwapora mali.

Waziri Dk. Gwajima alisema, vijana hao hawana uwezo wa kushindana na serikali iwapo wananchi watakuwa bega kwa bega katika kutoa taarifa za uhalifu na viashiria vyake kwa mamlaka za serikali.

"Hivyo wito wangu ni kwamba, shirikiane na serikali bega kwa bega kwa kutoa taarifa za uhalifu na viashiria vyake katika maeneo yao, ili kusaidia kukomesha vitendo hivyo ndani ya maeneo yetu," alisema Dk. Gwajima.

Alifafanua kuwa mshikamano wa wanajamii na serikali ndio suluhu ya kutokomeza vikundi hivyo vya vijana wanakadiriwa kuwa na miaka kati 16 hadi 20 ambao wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya uhalifu.

"Mmomonyoko wa maadili katika makuzi na malezi ni chanzo kikuu cha uzalishaji wa kundi hilo, kwani mtoto kuwa hivyo, sio suala la usiku mmoja, unakuta anaanza kidogo kidogo," alisema.

Waziri alisema, wazazi kwa upande wake hawatengi muda wa kuzungumza naye na kujua mienendo yake, anazidi kukuwa na tabia hiyo hadi anafikia hatua ya kujiunga katika makundi ya kihalifu kama hilo la 'panya road'.

Aidha, aliionya jamii kuacha kumwangalia mtoto kuwa ni wa mtu mwingine, badala yake watoto wote wahesabike kuwa ni wa wanajamii, wanapofanya makosa wawaonye au wawaadhibu ili kuwarudisha kwenye mstari.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, alisema amefarijika kusikia kuwa tayari vijana zaidi ya 61 wanaotuhumiwa kwa uhalifu wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kutokana na ushirikiano wa jamii. "Mwanzoni nilipokuja hapa kila mmoja wetu alikuwa na sura ya simanzi kwa hofu na woga uliokuwa umetanda, lakini leo mmeniambia tayari wapo ambao wanashikiliwa na vyombo vya dola, na wengine tayari wamefikishwa mahakamani kukabiliana na kesi zao, nimapongeze kwa hili," alisema Masauni.

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema, askari wataendelea kufanya kazi kwa mujibu wa viapo vyao bila huruma kwa atayethubutu kuchezea amani ya Watanzania katika kanda hiyo.

"Tumefanya kazi kwa ukaribu sana na Polisi Jamii, hawa wamekuwa msaada mkubwa na kutuwezesha kuwapata baadhi ya wahalifu hao katika maeneo ya Chanika, Kunduchi Mtongani na Kinyantiraa, ambapo baadhi ya watu waliokamatwa walikutwa na TV, simu na vitu vingine vilivyoporwa kwenye matukio hayo," alisema Kamanda Muliro.

# Mlezi TEHSA aona fursa katika utafiti

**Na Frank Monyo**

MLEZI wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Vyuo Wanaosoma Masomo ya Afya ya Mazingira (TEHSA), amewataka wanafunzi na wahitimu wa kada hiyo kuchangamkia fursa mbalimbali zilizoko kwenye sekta ya utafiti hususani kwenye eneo la usalama na afya mahali pa kazi ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Dk. Hussein Mohamed alitoa rai hiyo juzi mkoani Dar es Salaam katika jukwaa la kwanza la sayansi ya afya ya jamii na mazingira lililofanyika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili.

Jukwaa hilo liliwakutanisha wanafunzi wa vyuo, wahadhiri pamoja na wabobezi wa utafiti kutoka maeneo mbalimbali nchini ili kubadilishana uzoefu, elimu na fursa mbalimbali zilizoko katika sekta hizo.

Dk. Mohamed alisema: "Kuna fursa nyingi sana katika sekta hii ya afya ya mazingira kinachotakiwa ni mtafiti mwenyewe kuangalia tatizo liko wapi ili afanyie utafiti, mfano anaweza kuamua kufanya utafiti wa kubaini vihatarishi vilivyopo katika maeneo ya kazi."

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ndio waliofadhiliwa jukwaa hilo na kuandaliwa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili wakishirikiana na jumuiya ya wanafunzi wanaosoma masomo ya afya ya mazingira nchini.

OSHA waliwasilisha mada mbalimbali ikiwamo elimu juu ya masuala ya usalama na afya mahali pa kazi pamoja ili kuwajengea uelewa wanafunzi hao juu ya namna ya kutambua fursa mbalimbali watakapohitimu masomo yao.

Mkufunzi wa mafunzo hayo wa OSHA, Imakulata Longino alisema: "Baada ya kutoa mafunzo haya tunatarajia wanafunzi hawa watakuwa na uelewa mkubwa wa kutambua fursa mbalimbali zilizoko katika maeneo mbalimbali ikiwamo kuhamasika kufanya tafiti katika maeneo ya kazi na tafiti hizo tunaamini zinaweza kusaidia maeneo ya kazi, jamii na hata taasisi yetu kwa ujumla."

Mlezi wa wanafunzi wa kada ya afya ya umma na sayansi shirikishi Muhimbili, Prof. Gastro Frumence, aliishukuru OSHA kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha jukwaa hilo huku akitoa wito kwa wadau mbalimbali kuendelea kuunga mkono.

Rais wa TEHSA, Raphael Alphonce, alisema: "Kupitia OSHA tumeweza kuandaa jukwaa hili kubwa la kitaifa lililowakutanisha wadau kutoka maeneo mbalimbali nchini na tumepata fursa ya kujifunza mambo mbalimbali kupitia jukwaa hili ikiwamo elimu ya masuala ya usalama na afya kazini, lakini pia fursa zilizoko katika sekta ya utafiti, hivyo tunawashukuru sana na tunawaomba mwendelee kutuunga mkono."

Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kikishirikiana na TEHSA wamekuwa wakiandaa majukwaa mbalimbali kwa lengo la kukuza taaluma kwa wanafunzi hao kwa kuwakutanisha na wataalamu mbalimbali ili kubadilishana uzoefu, elimu na fursa katika maeneo mbalimbali.

# TARURA yajipa siku 30 kukamilisha daraja

**Na Mary Geofrey**

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Victor Seff, ametoa mwezi mmoja kwa watendaji wake wa Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, kukamilisha ukarabati wa daraja la Ifume.

Seff alitoa maagizo hayo juzi, wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya miradi ya barabara katika mkoa wa Katavi.

"Daraja hili ni muhimu sana kwa wakazi na kwa shughuli za kiuchumi, hivyo ni lazima mhakikishe kazi hii inakamilika kwa haraka ili wananchi wa Kalamsenga na Itunya kusafirisha mazao yao bila kupata usumbufu unaojitokeza kwa sasa, " alisema Seff.

Alisema TARURA makao makuu itatoa fedha ambazo alielekeza zitumike katika ukarabati wa daraja hilo na aliagiza tathmini ifanyike na maombi ya fedha hizo yatumwe ili yafanyiwe kazi kwa haraka.

Pia aliiagiza TARURA wilaya kuhakikisha inatoa haraka magogo na uchafu wote ulioletwa na mvua na kusababisha kuziba kwa daraja hilo ili fedha zikija ukarabati ufanyike ndani ya muda wa mwezi mmoja.

Naye Diwani wa Kapalamsenga, Jeff Lameck, aliushukuru uongozi wa TARURA kwa kusikia kilio chao kwa sababu wamekuwa wakipata adha kubwa kutokana na kuharibika kwa daraja hilo na alieleza kuwa wananchi watashiriki kikamilifu kuondoa magogo na uchafu katika daraja.

Kadhalika, Seff alikagua ukarabati wa barabara ya Kapalamsenga hadi Ifume kuelekea Bandari ya Karema, Tanganyika yenye urefu wa Kilomita 12.1 na kuridhishwa na kazi inavyoendelea na mpaka sasa ukarabati umefikia asilimia 90.

"Barabara hii itasaidia sana katika shughuli za usafirishaji wa mazao na pembejeo za kilimo na ni sehemu ya barabara ya kutokea Bandari ya Karema hivyo ni barabara muhimu sana," alisema Seff.




Mkurugenzi wa Biashara wa Halotel, Abdallah Salum (kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa na Masoko, Sakina Makabu, wakizindua kampeni ya "Taboa na Halotel 4G". **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wateja Halotel kujipatia fedha taslimu, simu janja

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Halotel Tanzania imezindua kampeni ya 'Toboa na Halotel 4G' kuwahakikishia wateja ubora na kasi ya mtandao wake kwa kuwapa huduma zenye ubunifu na kuendelea kuboresha mawasiliano nchini.

Pia imekuwa ikibuni bidhaa mpya zenye lengo la kuwazawadia wateja wake wanaotumia huduma za mtandao.

Mkurugenzi wa Biashara Halotel, Abdallah Salum amesema kampeni hiyo itawapa fursa wateja kushiriki katika promosheni hiyo itakayoendeshwa kwa wiki nane na washindi watapata zawadi mbalimbali zikiwamo fedha taslimu na simu janja.

"Ili kushiriki katika promosheni hii ya Toboa na Halotel 4G, wateja ambao wanatumia 3G wanaweza kubadili laini kwenda 4G bila gharama yoyote au mteja anaweza kusajili laini ya 4G na kuanza kutumia vifurushi vya intaneti kwa gharama nafuu na moja kwa moja atakuwa katika nafasi ya kuingia kwenye droo ya bahati na kuweza kuibuka mshindi," alisema Salum.

Pia, mteja anapaswa awe ameshatumia angalau 100 MB ndani ya siku tatu kuanzia siku aliyoanza kutumia mtandao wa 4G.

Alisema kampuni itawazawadia washindi 10 kila siku, kila mmoja atapata fedha taslimu Sh. 100,000.

"Kila wiki washindi watatu watazawadiwa simu janja ambapo mshindi wa kwanza atapata IPhone 13 pro max, mshindi wa pili atapata Samsung galaxy S22, na mshindi wa tatu atapata Samsung Galaxy A72," Salum alisema.

Vile vile, alisema kampuni imezindua kampeni hiyo kwa kuzingatia tayari mtandao wake wa 4G umeenea katika maeneo mengi na kwa sasa ina vituo vipatavyo 1,037 vinavyosambaza mtandao wa 4G na mtandao wa 4G umeongeza nguvu na ufikiaji wa maeneo mengi ya nchi.

Alisema sababu nyingine ya kuanzisha kampeni hiyo ni kuwapa wateja uzoefu wa ubora wa 4G huku ikiwapitia zawadi mbalimbali, na hivyo kufanya huduma hiyo kuwafikia Watanzania wengi zaidi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kwa sasa mtandao wa 4G umewafikia asilimia 45 ya Watanzania.

"Hii ni kutokana na kukua kwa huduma za kidijitali hapa Tanzania na kuongezeka kwa uhitaji katika soko, na hivyo uwekezaji mkubwa wa kampuni umeelekezwa kwenye miundombinu katika juhudi za kuongeza vituo vya usambazaji mtandao wa 4G," alisema Salum.

Kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita kampuni imekuwa ikijielekeza katika mikakati ya kupanua wigo wa mtandao wake hapa Tanzania. Salum alisema kwa kuzingatia kuwa asilimia 30 ya wateja wake wanatumia mtandao wa intaneti, kampuni inapanga kuongeza idadi hiyo kufikia asilimia 40 ifikapo mwisho wa mwaka huu.

Halotel tayari imeanza kuzindua kizazi cha nne cha huduma za mtandao wa 4G katika maeneo mengi ya nchi.

# Tril. 6.5/- kusambaza umeme vitongoji vyote vya Tanzania

BUNGE limeelezwa kuwa serikali inatarajia kutumia Sh. trilioni 6.5 kwa ajili ya kuhakikisha vitongoji vyote nchini vinapata umeme.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Stella Fiyao.

Katika swali lake, Fiyao alihoji serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inaweka umeme katika vijiji na vitongoji vyote nchini.

"Serikali imetangaza kiasi cha Sh. 27,000 kwa ajili ya unganishaji wa umeme vijijini. Ni lini vitongoji vyote nchini vitapatiwa umeme ili kuwawezesha wananchi kupata maendeleo?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Byabato alisema ni nia ya serikali kuhakikisha maeneo yote nchini, vikiwamo vitongoji, yanafikiwa na umeme.

"Kutokana na hali hiyo serikali imetenga Sh. trilioni 6.5 kwa ajili ya kufikisha umeme kwenye vitongoji vyote," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vijiji vyote vya mkoa wa Songwe vinapata umeme wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo aliosema mkoa wa Songwe una vijiji 307, vijiji 180 vina umeme na vijiji 127 ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme.

"Vijiji hivyo 127 ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme vinanufaika kupitia mradi wa REA III mzunguko wa pili unaoendelea," alisema.

Aidha, alisema utekelezaji wa mradi unaendelea na mkandarasi Derm Electrics anayetekeleza mradi kwa kipindi cha miezi 18 kwa gharama ya Sh. bilioni 11.23 na mradi huo unatarajiwa kukamilika Desemba, mwaka huu.



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa (kushoto), akijadiliana jambo na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dk. Stergomena Tax (kulia) pamoja na Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassoro Mbarouk, ndani ya ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Muswada bima ya afya karibu kuiva

WIZARA ya Afya iko katika hatua ya ukamilishaji wa Muswada wa Sheria wa Bima ya Afya kwa Wote ambao utawezesha kurahisisha huduma ya upatikanaji wa bima za afya kwa wananchi wote.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi aliyaetaka kujua serikali kwa nini kadi za bima ya afya zinachelewa tangu mteja anapokuwa amejiunga.

"Katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna ucheleweshaji wa kadi za bima ya afya hadi kufikia miezi sita tangu mwanachama anapojiunga," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo aliitaka serikali ieleze ina mpango gani wa kutoa kadi ya bima ya afya kwa njia ya kifurushi kikubwa kwa ajili ya kutoa matibabu kwa wagonjwa wa figo.

"Serikali ina mpango gani wa kurahisisha huduma ya upatikanaji wa bima ya afya kwa wananchi wake?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Mollel, alisema kadi za bima ya afya kuchelewa kuanza kazi kwa muda wa miezi mitatu hadi sita tangu mwananchi anapojiunga ni tatizo.

"Kadi inatakiwa kupatikana ndani ya miezi mitatu na tatizo kubwa ni pale ambapo watu wanapokuwa na afya hawakumbuki kujiunga na kadi ya bima ya afya mapema," alisema. Kutokana na hali hiyo, Dk. Mollel alisema serikali iko katika hatua ya ukamilishaji wa Muswada wa Sheria wa Bima ya Afya kwa Wote ambao utawezesha kurahisisha huduma ya upatikanaji wa Bima za Afya kwa wananchi wote.

## Ruzuku ya kahawa kuanza kutolewa

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali ina mpango wa kutoa ruzuku kwa zao la kahawa kama yalivyo mazao mengine.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Esther Maleko, ambaye alisema katika mikoa 15 nchini ikiwamo Kilimanjaro, Kagera, Tanga na Ruvuma ambayo uchumi wa mikoa hiyo unategemea kahawa lakini haina ruzuku kama yalivyo mazao mengine ya kimkakati.


"Je, ni nini msimamo wa serikali kuhakikisha zao hili linapata ruzuku kama mazao mengine?" Alihoji.

Akijibu swali, Majaliwa alisema kahawa ni miongoni mwa mazao yanayotegemewa kupandisha uchumi katika maeneo mbalimbali nchini.

"Katika kuhakikisha umuhimu wa zao hili nchini, hivi karibuni nilikuwa mkoani Kagera kushughulikia zao hili lakini jana (juzi) Wizara ya Kilimo imekamilisha bajeti yake ambayo pia wabunge wengi katika mijadala yao walizungumzia ustawi wa zao hili," alisema.


Alikiri kuwa serikali inao mkakati wa kutoa ruzuku kwenye mazao mbalimbali inayotegemea mahitaji ya zao husika kama vile mbegu, dawa, pembejeo na namna bora ya kulisimamia zao hilo husika.

"Zao la kahawa na lina mahitaji tunayofanyia ruzuku. Pia linahitaji miche na dawa. Kagera tunatoa ruzuku kwenye miche pia tumekubaliana na waziri kujenga maghala kule Kagera. Ruzuku itakapokuja itajua mahitaji ni nini tutaoa ruzuku kutegemea na mahitaji ya zao na eneo," alisema.




Habari zote na Augusta Njoji

Ukurasa 13




Watanzania tulipie elimu au matibabu?

BUFE
IJUMAA MEI 20, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



**SIKU YA ASALI DUNIANI**
**TFS Kanda ya Ziwa: Tuna utajiri huu wa nyuki, hii hapa mikakati yetu itakayotuibua kitaifa**

Ukurasa 12

# FAO inavyowaondoa wanawake Kigoma kutoka wategemezi, hadi wanaohudumia

## • Siri ya majibu iko ndani ya shamba lao

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA sasa iko katika mageuzi makubwa ya kuwainua kinamama kufika kwenye usawa na haki. Nadharia iliyoko kimataifa kuanzia Umoja wa Mataifa (UN), hadi kitaifa ikiwamo nchini.

Inapozungumzwa mageuzi, pia inajumuisha maisha ya mtu mmoja mmoja, kiuchumi. Hapo ndipo nyenzo za UN nazo zinafuatilia moja kwa moja, ikiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO), likishughulikia, ushuhuda nchini ukiwamo mkoani Kigoma.

Mnufaika mwanamama, Grace Ntazika, mkazi wa Kijiji cha Kitahana, kilichoko kata ya Kitahana wilayani Kibondo, sasa anafurahia akitamka "wanawake tuondokane na fikra za utegemezi kwa wanaume. Wakati huu wa sasa, wanawake na utegemezi na kuwa imara kiuchumi."

Mkulima Grace katika ushauri wake anaenda mbali akisisitiza kuwa siyo wakati wao kulala tena kuwategemea wanaume, bali wasimame wenyewe ana anajigamba kwamba imethibitika mwanamke akifanya chochote iwe biashara, kilimo au uongozi, huwa na umakini zaidi.

Mwanamama huyo mkulima, ni mnufaika wa mafunzo ya FAO yanayoendana na kupatiwa stadi za kisasa za kilimo, matumizi ya mbegu za kisasa zinazohimili mabadiliko ya tabianchi, pia samadi zinazowajengea uwezo wakulima wote.

Ni aina ya simulizi inayotolewa, kwenye mfano hai huku anapukuchua mahindi aliyoyavuna msimu huu wa mwaka 2022. Anakiri yako bora maradufu kuliko ya mwaka jana, sababu kuu ni aina ya mbegu anayoitaja kwa jina 'Njano Uyole' aliyopatiwa na FAO.



Wanufaika wa kilimo bora mkoani Kigoma, wakihudumia mavuno yao. **PICHA: MTANDAO.**

"Ushauri wangu ni kwamba wanawake wenzangu wajiunge na vikundi ili wapate mbinu bora za kilimo cha kisasa, hatimaye waondokane na kero za kila siku za kuwa na fikra za utegemezi kwa kinababa. Ukijiunga na vikundi vya ushirika na vile vya kilimo, lazima utapata fedha za kujikimu kwa mahitaji mbalimbali," anashauri Grace.

Mama huyo yumo katika kikundi wa 'Umoja ni Nguvu na Mshikamano A' kutoka kata ya Katanga wilayani Kakonko, Kigoma wanakolima maharage aina ya Jesca yenye virutubisho asilia vya madini ya chuma, kutoka shamba darasa lao lililofanikishwa na mafunzo ya mradi wa pamoja wa Kigoma wa UN kupitia FAO.

Hadi sasa inaelezwa nchini Tanzania hususani mkoani Kigoma, kuwa mafunzo hayo ya kilimo, yamewajengea wanawake uwezo na sasa wanakidhi mahitaji yao, pia kulipa gharama za pembejeo za kilimo.

Anakiri kuwa mbegu ya Njano Uyole imekuwa bora kuliko nyinginezo alizowahi kutumia, akifafanua: "Wakulima kupitia Chama cha Ushirika cha Kitahana, tumepata bahati ya kulima ekari 40.

"Kila mkulima ana uhakika wa kupata fedha ya kulipa deni la pembejeo na kubaki na masalia ya fedha anayoweza kujikimu, pia kusomesha watoto," anasema Grace.

Wakulima hao wanatajwa mbali na kuuza maharage kupata fedha, pia wanautumia kwenye mlo ikiwa manufaa hata kiafya - protoni, kwa wale wajawazito huku zao hilo likiwa na sifa ya kurutubisha udongo, yanakomaa mapema, pia kuvumilia magonjwa.

### UFUGAJI WA KUKU

Aina hiyo ya manufaa ndio yanatajwa kuwafikia wanawake wa maeneo kama ya Twabagondozi wilayani Kibondo mkoani Kigoma, baada ya kuhangaika muda mrefu wakipoteza mayai na mara nyingine kuyauza kwa bei ya chini, kwani hawakuwa na uhakika wa kutotolesha mayai, kwa kukosa vifaa vya kisasa vya kazi hiyo.

Grace anasema, hatimaye wafugaji kuku nao wameanza kuona nuru FAO ilipowaletea mashine ya kutotolesha vifaranga, kwali awali wafugaji wengi wamehangaika muda mrefu kwa kukosa vifaa bora.

Pauli na Ezron ni mkazi wa eneo hilo, anatoa ushuhuda wake kwamba, licha ya kutokuwa mwana kikundi, lakini yuko jirani na kikundi cha Twabagondozi wilayani Kibondo, akieleza namna anavyonufaika nacho:

"Hapa nimekuja kuchukua vifaranga ambavyo nilileta mayai 10 kutoka katika banda langu na nimeweza kupata vifaranga vinane. Nimepata huduma ya kutotoleshewa mayai kupitia kikundi cha Jipe Moyo."

Mmoja wa wanakikundi, Essau Masunzu, anafafanua kuwa wanatotoa vifaranga kutoka kwenye mayai yaliyotagwa na kuku wa kikundi, pia wanawatotoleshea watu wengine na jamii inayowazunguka kwa bei Sh. 500 kwa kila yai.

"Tulikuwa tunauza yai moja kwa shilingi mia tano, lakini sasa yai hilo tunalibadili na kuwa kifaranga, tunauza kwa takribani Dola moja ya Kimarekani (Sh.2,400) kwa kifaranga kimoja," afafanua.

Programu ya pamoja kwa mkoa wa Kigoma ilianza mwaka 2017 na mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayohusika ni pamoja na lile Chakula na Kilimo, FAO, Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Kituo cha Biashara cha Kimataifa (ITC) na Shirika la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF).

***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa mbalimbali, ikiwamo za Umoja wa Mataifa nchini kuanzia mwaka jana.***

BIASHARA

MAADHIMISHO SIKU YA NYUKI DUNIANI

# TFS Kanda ya Ziwa: Tuna utajiri huu wa nyuki, hii hapa mikakati yetu itakayotuibua kitaifa

• Kaulimbiu: Nyuki ni Uchumi, Tuwalinde na Tuhifadhi Mazingira yao

**Na Anthony Gervas, Mwanza**

KATIKA jitihada za kupanua fursa ya upatikanaji asali, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Ziwa, unaendelea kuboresha sekta ya ufugaji nyuki kwa kuongeza thamani na kiwango cha uzalishaji wa mazao yake, utakaokuwa na tija katika kipato cha mtu binafsi na taifa.

Kama ilivyo kaulimbiu ya Siku ya Nyuki Duniani inayoadhimishwa leo 'Nyuki ni Uchumi Tuwalinde na Tuhifadhi Mazingira Yao' lengo lililopo ni kuenzi na kuendeleza mchango wa viumbe hao katika usalama wa chakula na uchumi.

Vilevile, kuna suala la uhifadhi wa mazingira na uendelezaji baioanuai, kazi zinazofanyika kutekeleza Sheria ya Ufugaji Nyuki ya Mwaka 2002, Kanuni za Ufugaji Nyuki za Mwaka 2005, sambamba na sera yake ya mwaka1998 iliyoboreshwa mwaka jana.

Nyuki kimaumbile wanaelezwa kuwa na jozi ya mabawa, wakiishi kwa ujamaa wanatengeneza asali, wakiwa wa aina mbili. Wapo wenye umbo kubwa wanaouma na wadogo wasiouma, ambao ni nadra kupata asali yao. Nyuki hufugwa kwenye maeneo yanayoitwa manzuki.

Mhifadhi na Msimamizi wa Kitengo cha Nyuki, kutoka TFS Chrisman Rugundu, anaelezea zaidi aina tatu za nyuki katika mizinga ya kufugia.



Mizinga ya nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali, iliyotegwa porini. **PICHA: MTANDAO.**

**MALKIA NA KIBARUA**

Rugundu anasema kwenye mzinga wa kufuga kuna nyuki malkia anayeongoza wezake na kazi yake kuu ni kutaga mayai, akiwa na wajibu kuhakikisha kundi lililopo linabaki kufanya kazi zake. Pia, anataja kuwapo nyuki dume, kazi yake kubwa katika mzinga ni kumzalisha malkia.

Mhifadhi Rugundu anaendelea: "Kuna nyuki mwingine maalum ambaye ni kibarua anayefanya kazi kubwa ya ulinzi, kutengeneza chakula kama vile asali, kutengeneza masega,n'ta, kufanya mawasiliano pamoja na usafi, lakini kwenye kundi moja huwa kuna idadi ya nyuki kuanzia 20,000 hadi 80,000 katika mzinga."

Ili kupata tija katika ufugaji nyuki, anasema kunapaswa kuzingatiwe kalenda ya ufugaji yenye mwongozo unaomsaidia mfugaji kujua majira na kazi zinazotakiwa kufanywa au wajibu wake, ambao umegawanyika katika misimu minne.


Anaanza kuutaja msimu wa njaa, anaoufafanua upo katika kipindi cha kiangazi, penye ukame na mimea, unapukutisha maua na majani yake, ikiendana na matokeo kuwapo chakula kidogo kwenye mzinga na idadi ya nyuki kupungua.

Rugundu anasema ni katika kipindi hicho malkia wa nyuki ama anapunguza au kuacha kutaga mayai kabisa, makundi ya nyuki yanahama kutafuta sehemu zenye malisho (ubichi) baadhi yake hupita kwenye kundi la nyuki na kuiba asali.

**MSIMU WA UJENZI**

Ni msimu unaoanza kwenye mvua za awali, mimea kuchanua kwa wingi, hapo makundi mengi yanatafuta makazi na kuzunguka kwenye mizinga sehemu nyinginezo.

Aidha, nyuki hujenga masega ya asali na wanazaliana kuongeza idadi yao kwenye mzinga, makundi yakipita kutafuta mahali pa kuishi na kuhama, endapo kuna maadui au la kama mzinga wao umekuwa mbovu.



Meneja wa Wakala wa Huduma za Misitu Kanda ya Ziwa (TFS), Bakari Mohamed, akiwa ofisini kwake jijini Mwanza.



Mhifadhi na Msimamizi wa Kitengo cha Ufugaji wa nyuki, kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Kanda ya Ziwa(TFS), Chrisman Rugundu. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

Rugundu anaeleza, kwamba mfuga nyuki anatakiwa kukagua mizinga iwe katika hali ya usafi na wakisafisha na kuandaa mizinga isiyokuwa na nyuki, pia anatafuta nyuki, wanatundika mizinga ya kukamata makundi mengine katika sehemu wanakopita.

Lingine analitaja ni kuzalisha makundi na kusaidia nyuki kuongeza kiota kwa kuweka sanduku la ziada, wakihakikisha wana chakula cha kutosha, wanakagua mizinga ya kisasa ya viunzi na kuvuna uliobebeshwa endapo una asali iliyokomaa, kutembelea kila mara makundi ya nyuki kuona maendeleo yake au matatizo.

**MSIMU WA MTIRIRIKO**

Rugundu anaeleza kwamba katika msimu wa mtiririko wa asali, ni kipindi ambacho miti na vichaka vimechanua maua kwa wingi na nyuki wanatembelea kukusanya.

Hapo anasema wanakusanya mboji na kubadilisha kuwa asali, lakini maadui wao ni wadudu kama sisimizi na siafu. Wanatengeneza masega, wakitafuta maji na kuweka kumbukumbu za maendeleo.

Katika hilo inaelezwa mfugaji hutakiwa kujenga ushirikiano na wafugaji jirani kushughulikia changamoto zinazojitokeza, vilevile ni wajibu wa mfugaji katika msimu anakagua mizinga, pia anafyeka majani na matawi ya miti sehemu husika.

Lingine analitaja ni kuwekwa masanduku ya ziada yanayobebesha mizinga hata kuongeza uzalishaji na kufanya maandalizi ya vifaa vya kuvuna na kuhifadhia asali, ikiendana na kutafutwa masoko ya asali, kukiwekwa kumbukumbu za kila kundi ulilovuna.

Msimu wa mavuno kwa mfugaji ni wakati ambao maua ya mimea yamepungua na kuanza kutoa ama mbegu au matunda, kwa maana ya mwanzo wa kiangazi.

Wajibu mmojawapo wa mfugaji, anataja ni kuvuna masega yenye asali iliyokomaa kwa kutumia bomba la moshi na mavazi ya kinga, wakiwa na vyombo safi wakichuja asali na kuiweka katika sehemu sahihi na salama.

Kimsingi, mazao ya nyuki yanajumuisha asali, n'ta na gundi, huku ikimpatia binadamu kipato, chakula kisichoharibika na tiba na mazao lukuki kunufaisha viwanda vya kutengeneza urembo, dawa na chakula.

Vilevile, anataja athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira katika ufugaji nyuki ikiwemo kilimo kinachotumia kemikali, kinachosababisha wadudu hao kuuawa.

**MENEJA KANDA YA ZIWA**

Meneja wa Wakala wa Huduma za Misitu Kanda ya Ziwa (TFS) Bakari Mohamed, anaeleza majukumu yao ni pamoja na kulinda misitu ya asili iliyohifadhiwa kwa miaka mingi, sasa ikiwa chini ya uangalizi wa serikali isiharibiwe na jamii.

Mohamed anasema, ipo haja ya jamii, taasisi binafsi na viongozi wa sekta za umma na wanasiasa, kuweka nguvu ya pamoja kuhakikisha hifadhi za misitu zisitoweke.

"Jukumu letu kubwa ni kulinda misitu ya asili iliyoachwa tangu enzi za ukoloni, kuziendeleza hifadhi za misitu zilizopo, ili zisitoweke kutokana na shughuli za kibinadamu ambazo ni ukataji miti ovyo, uchomaji mkaa, kuchoma moto, vikiwemo vyanzo vya maji kuharibiwa," anafafanua.

Meneja huyo anataja kuwepo msitu kunarekebisha hali ya hewa kwa kufyonza uchafu, ikiwanusuru binadamu dhidi ya magonjwa ya ngozi na kansa.

**MIKAKATI IKOJE?**

Meneja huyo anasema mikakati yao ni kuendelea kuhifadhi misitu ya asili, kupanua maeneo ya uhifadhi wa taifa, kuanzisha mashamba ya miti kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi, ikiwemo kukuza sekta ya ufugaji nyuki kwa kuanzisha hifadhi za nyuki.

Anasema katika hilo, wataendelea kutoa elimu katika jamii, kuongeza kasi ya upandaji miti katika halmashauri zote za mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuboresha mashamba ya misitu inayohifadhiwa na serikali.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Watanzania tulipie elimu au matibabu?






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

TANZANIA ni mahali pazuri sana pa mtu kuishi, kwani ndipo unaweza kusikia hoja inaibuliwa na kujadiliwa kwa nguvu kubwa, na kisha kufa kifo cha mende na kusubiri kipindi kingine cha mwaka kuwadia.

Hivi sasa katika kipindi hiki cha mkutano wa Bunge la Bajeti,

ndipo utasikia masuala mbalimbali yakijadiliwa kwa nguvu kubwa na ubishani mkali baina ya wabunge na mawaziri, yaani wananchi na serikali yao.

Lakini, mkutano huu utakapomalizika na kila mtu kurudi anakostahili kuwa, yote yanakuwa kimya na inaibuka hoja nyingine mitandaoni, inayotawala mawazo ya Watanzania hawa na kusahau hata umasikini wao.

Nimekuwa mmoja wa wenye kiherehere cha kusikia nini kinajadiliwa bungeni na wawakilishi wetu na kujibiwa na mawaziri. Yapo yanayovutia na kufurahisha, lakini mengine ni ukakasi.

Hata hivyo, hunipa kianzio cha name kushughulisha akili yangu ambayo pengine inaweza isivuke mipaka na kubakia kwangu na kusaidia kidogo familia niliyojitengenezea kwa makusudi.

Nimekuwa mara kwa mara nikipenda sana kusikiliza hoja kuhusu huduma za jamii, hususan za elimu na afya. Ndiyo sababu hupenda sana kumsikiliza Mbunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba, maarufu Profesa.

Mbunge huyo hukaa kimya akisikiliza wengine, lakini anapopewa fursa ya kusimama kuzungumza, kila mmoja hujikuta akihoji halmashauri ya kichwa chake, kama alisikia vizuri na kuamua kuzingatia au la, kutokana wa staili ya anachowasilisha.

Mimi huzingatia sana maneno yake yanayolenga kuangalia mustakabali wa elimu nchini, kama inawasaidia wanetu katika kujikomboa wao na kutukomboa sisi wazazi wao, lakini Taifa kwa ujumla.

Hatimaye ukimsikiliza vizuri Kishimba, utaona elimu tunayopeana hapa nchini, haina tofauti na kutwanga maji kwenye kinu, tunaishia kujilowanisha tu wenyewe bila kunufaika na chochote.

Hiyo inaonyesha ni jinsi gani hatujipangi tukawa na dira au mwelekeo unaoeleweka utakaotupa tija katika elimu tunayopeana, licha ya kuwa na mikutano ya Bunge kila mwaka.

Hoja yake, ni kwamba tunapeleka wanetu shuleni wanasoma na kuhitimu, lakini hatimaye wanarudi majumbani kukaa kama walivyokuwa kabla hawajaanza shule. Maana yake tunapoteza muda kusoma na kusomesha.

Ukitafakari sana na ukaona vijana wangapi waliohitimu elimu zao na kuoanisha na wanachokifanya sasa, huku wakubwa wakiwahimiza kujiajiri kana kwamba shuleni walifundishwa kujiajiri, utashangaa.

Hapo ndipo nami nakuja na mawazo yangu na kujiuliza kama kati ya elimu na afya nini kinatakiwa kutolewa bure kwa watu, najikuta natetea afya iwe bure kuliko elimu. Wazo hilo halinifanyi kupinga sera ya Dk. John Magufuli (alazwe pema) ya elimu bila malipo, ingawa kuna vijimalipo vinafanywa na baadhi ya shule, lakini kama hakuna faida hata ukisoma bure ukarudi nyumbani, ndiyo nini?

Watu husema bila elimu huwezi kumpata daktari anayekutibu, lakini elimu ya leo hii ina maana gani, kama hata hao madaktari wanamaliza, lakini wakarudi mitaani kutafuta ajira na kuambiwa jiajirini?

Pia, kama sifa ya kuwa mbunge mpaka leo ni kujua kusoma na kuandika, kuna sababu gani ya mtoto kuzeekea shuleni na vyuoni na kurudi nyumbani kuungana na wazazi wake, kwa kukosa mahali pa kwenda kutumikia alichosoma?

Ukikosa elimu si rahisi kufa, lakini ukikosa huduma ya afya ni rahisi kufa. Tunajua wengi wetu ni masikini, sasa je tujiulize hicho kipato tunachokipata kutokana na juhudi binafsi, tukipeleke shuleni au hospitalini?

Kwa akili hii ninayotumia kuandika hapa, mimi ningependekeza shuleni tujilipie, lakini hospitalini tulipiwe. Yaani ile pesa inayotolewa kila mwezi shuleni chini ya sera ya elimu bila malipo, iende hospitalini kwa sera ya tiba bila malipo.

Hiyo itafanya watu wasiendelee kusumbuliwa na maradhi ambayo si rahisi mtu kupambana nayo, kuliko kupambana na ujinga ambao unaweza kuondoka hata kwa watu kueleweshana tu hiki kibaya na hiki kizuri, na si ugonjwa. Kwa sababu naona hili la bima ya afya ni kizungumkuti. Alamsiki!

UCHUMI

MOSES NTILEMA:

# Mtaalamu bingwa wa bahari ahitaji mageuzi sasa kuwepo utalii fukwe

## • Ni mwendelezo wa Uchumi Buluu

**Na Renatha Msungu,**

**DODOMA**

UTALII wa fukwe ni moja ya maeneo muhimu ambayo Tanzania bado inaelezwa haijawekeza vya kutosha.

Moses Ntilema, ni mwanamichezo wa uokoaji kwenye maji na mtaalamu wa shughuli za usalama na uokoaji majini ndani na nje yaTanzania tangu 2008, anaeleza kuguswa na umuhimu wa Uchumi wa Buluu kupanuliwa katika mustakabali mpana.

Ntilema anasema alianza mafunzo yake ya uokoaji majini nchini Kigamboni Dar es Salaam, kisha akajiendeleza katika nchi tofauti, ikiwamo Afrika Kusini

ambako ndiko anakofanya mafunzo zaidi ya uokoaji majini.

Ntilema anaieleza Nipashe shauku yake kubwa kuona Tanzania inapiga hatua katika michezo ya uokoaji majini, pia anaguswa na harakati za kuiweka nchi katika uchumi wa buluu, hasa katika eneo la utalii wa fukwe.

Anaioanisha na namna ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu, kutangaza utalii wa nchi kupitia filamu iliyozinduliwa hivi karibuni ya kutangaza utalii, Royal Tour.



Sehemu ya ufukwe wa Zanzibar, ambao unatajwa una sifa ya kutumiwa kwa utalii wa ufukwe na kuwa chanzo kikubwa cha mapato. **PICHA: MTANDAO**

### UCHUMI BULUU ULIVYO

Ntilema anabainisha kuwa, uchumi wa buluu umegawanyika katika vipengele muhimu 14, ikiwa ni uvuvi, uhifadhi viumbe bahari, viwanda vya samaki, uundaji wa meli, bandari.

Mengine anayaorodhesha kuwa ni nishati ndani ya bahari, usafirishaji majini, utalii majini, majisafi, utunzaji mazingira, nishati ya upepo, nishati mawimbi maji, nishati ya kibaiolojia, na kilimo cha majini.

Anafafanua, ili uchumi huo wa buluu uweze kukamilika nchini na kuwa wenye faida endelevu, unahitaji mambo muhimu anayoyataja kuwa ni taaluma au wataalamu wa kutosha hasa kutoka nchi husika, pia miundombinu.

Mtaalamu huyo, pia anataja mengine ni; usalama na utulivu baharini; utunzaji na ulindaji mazingira; mipango thabiti ya baharini; ulinzi wa bahari; ukusanyaji wa taarifa; usawa katika matumizi ya bandari; na usawa wa shughuli za uvuvi.

"Nchi za kwanza kupata na kufaidika na uchumi wa buluu duniani ni nchi za Bara la Ulaya kama Hispania, Ujerumani, Italia, Ufaransa, Ureno na

Uholanzi, Afrika nchi ya kwanza kunufaika na uchumi wa buluu kwa kiwango cha juu, ni Misri hasa katika ule mradi wao wa Mlango Bahari wa Suez Mpya (New Seuz Canal) wa mwaka 1869 uliokuwa njia kuu ya pili ya dunia ya mlango bandari," anafafanua.

Anasema, mataifa makubwa kama Marekani, China, Australia na Japan, yamekuwa yakiongeza juhudi kufaidika na uchumi wa buluu, sambamba na nyinginezo; Indonesia na Singapore.

Mnamo mwaka 2016, inalaezwa iliweza kutengeneza ajira zaidi ya milioni nne duniani kote, Hispania peke yake ikizalisha ajira 700,000, kufuatiwa na Ujerumani na Uingereza, zenye jumla ya ajira 400,000 hasa kupitia nishati ya umeme.

### UZOEFU KIMATAIFA

Ntilema anasema, Zanzibar kwa sasa ni miongoni mwa visiwa bora vyenye vivutio vingi duniani hasa kwa utalii wa baharini na fukwe zake.

Akiwa na uzoefu kazi ya msimamizi wa fukwe katika nchi tofauti ndani duniani, anasisitiza kuwa amejifunza mengi, akipanyooshea kidole Zanzibar kuwa na maeneo inayoweza kuyafanya utalii fukwe pasipo kutegemea wawekezaji wageni, ambao wengi vipaumbele vyao ni faida kwanza.

Ntilema anarejea sehemu ya taaluma yake kwenye utalii wa majini ma mahsusi, uboreshaji fukwe za bahari na vivutio vyake, nchi nyingi kubwa duniani zilianza kusimamia fukwe zao miaka ya nyuma

akitoa mfano wa Australia iliyoanzia mwaka 1907, huku barani Afrika, Afrika Kusini ikaanza mwaka 2013.

### NINI KIFANYIKE Z'BAR?

Hapo akiwa mtaalamu ametoa rai kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kulipa kipaumbele suala hilo kwani uchumi wa buluu, hutegemea sana suala la usalama majini, ambako kunawavutia watalii na wawekezaji wengi.

"Kutokana na tafiti zangu za uchumi wa buluu duniani, mfano mwingine wa kuigwa ni kutoka nchi au kisiwa cha Grenade, St. Vincent, Maldives na Costa Rica.

"Grenade, nchi isiyokuwa na majeshi kama mataifa mengine...iliwekezwa katika kuboresha fukwe kama kitovu cha utalii, kuboresha huduma za afya na elimu.

"Nimeshuhudia kwa macho yangu namna gani nchi nyingine huingiza mapato makubwa kupitia utalii wa fukwe ambao kwa Afrika pekee nchi

kama Afrika Kusini, Misri na Morocco, utalii wa fukwe umechangia kwa kiasi kikubwa na kuzifanya nchi hizo kuwa na kiwango kikubwa barani Afrika, kwa kuingiza watalii zaidi ya milioni 11 kila mwaka," anaeleza Ntilema.

Anasisitiza kuwa, uwekezaji wa fukwe unaweza kufanywa na Serikali ya Mapiduzi Zanzibar kwa gharama nafuu, yenye faida kubwa, hasa kwa kuwatumia wataalamu wa ndani, kwani wao uwezo wa kufahamu undani zaidi, jiografia ya nchi na changamoto zake.

"Zanzibar ina fursa ya kuwa na fukwe yenye hadhi ya kimataifa yaani 'Blue flag Beach' ambayo itakuwa ya kwanza ndani ya Afrika Mashariki," anasema na kufafanua, itaongeza ushindani zaidi wa uchumi wa buluu na mataifa mengine ya jirani.

Ntilema aliyebobea kimataifa, anarejea nchi na visiwa vya Maldives na Seychelles, zimepiga hatua kubwa kwa kutoa huduma bora za kijamii, kwa kutegemea pato litokanalo na uchumi wa buluu kupitia fukwe zake baharini.

Pia, anasema mataifa makubwa yamekuwa yakiwatumia sana wadau na wataalamu wao wa ndani wa usalama na uokoaji majini katika kuboresha utalii wa fukwe, hivyo Zanzibar inaweza kupata watalii wengi zaidi katika

kipindi kilichopo cha migogoro kimataifa na mabadiliko ya tabianchi, nyakati za joto watalii hupenda sana kwenda kwenye fukwe za bahari hasa visiwani.

### NTILEMA NI NANI?

Kwa vipindi viwili amekuwa Mtanzania wa kwanza kusimamia mashindano makubwa ya mchezo maarufu duniani ndani ya mji mdogo wa Port Elizabeth, Afrika Kusini akishuhudia washiriki 2,800 na wageni zaidi ya 5,000 katika mashindano hayo ya duniani.

"Na moja ya sifa kuu ya kuwa mwenyeji wa mashindano hayo ni kuwa na fukwe nzuri, miundombinu bora na usalama majini hivyo, anaamini kabisa moja ya ndoto yake ni kuona Zanzibar inakuwa wenyeji wa mashindano

hayo miaka michache ijayo inaweza kutimia," anasema.

Sasa Ntilema anakusudia kuitumia vema taasisi yake mpya ya Tanzania Lifeguarding Center katika kutoa mchango kwa serikali ya Zanzibar, katika kuleta mabadiliko makubwa ya uchumi wa buluu kupitia utalii wa fukwe.

Pia, anasema alishiriki pia katikaa uokoaji pale ilipozama

meli ndogo ya Spice Islander mnamo Oktoba 10 mwaka 2011 na Mv Skagit mnamo Julai 18 2012 kisiwani Chumbi Zanzibar, akiwa mwakilishi kutoka chama cha skauti.



## Serikali yapania kuibua wabunifu vijijini

Na Renatha Msungu, DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema serikali itajikita zaidi kufika maeneo ya vijijini kuibua wabunifu watakaoleta bunifu zenye tija katika kutatua vikwazo vya kilimo.

Prof. Mkenda alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akifungua mdahalo ulioandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) katika wiki ya ubunifu inayoenda sambamba na mashindano ya taifa ya ubunifu nchini (MAKISATU).

Prof. Mkenda alisema kuna wabunifu mbalimbali wasiojulikana mitaani na lengo la serikali ni kutangaza na kuwaibua wabunifu hao kutoka maeneo ya vijijini ikiwamo shule ili kuleta ufanisi wa ubunifu hapa nchini. "Serikali haiwezi kuwatelekeza wabunifu, bali inafanya jitihada ya kuendeleza bunifu zinaibuliwa ili wasonge mbele," alisema Prof. Mkenda.

Alisema wabunifu wenye vipaji wanapaswa kujitokeza ili kuonyesha kazi zao ambazo zitagawa kazi na baadaye zitaendelezwa kupitia hatua mbalimbali.

Aidha, Prof. Mkenda alisema sio kila ubunifu unahitaji fedha na kutoa wito kwa wabunifu kutangaza bunifu zao ili waweze kutambuliwa na bunifu zinazohitaji fedha serikali itaendelea kusaidia wabunifu ili kuinua bunifu zao.

Alisema ni muhimu kuendeleza wabunifu kwasababu dunia inabadilika na ubunifu unafanywa na watu wa rika mbalimbali ikiwamo watoto.

Awali, Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amosi Nungu, alisema wiki ya ubunifu ni sehemu muhimu kwa kuendelea kuchagiza ubunifu wenye tija katika maendeleo ya nchi, pia inatoa nafasi kubwa kwa wabunifu kuendelea kujuana katika kupanua bunifu wanazozifanya.

Alisema walichogundua ubunifu mwingi uko mtaani unahitaji kuibuliwa.

# Wabunifu waipongeza serikali kuwapa fursa

Na Paul Mabeja, DODOMA

WABUNIFU nchini wameipongeza serikali kwa kuweka mazingira wezeshi ya kuonyesha bunifu zao mbalimbali kupitia maonyesho ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU).

Mbunifu wa kifaa cha kupima kiasi cha gesi kwenye mitungi (CLICK GAS) Joshua Joasi, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho hayo yanayofanyika jijini hapo kwa muda wa wiki moja.

Alisema wanaishukuru serikali kwa kuwezesha maonyesho hayo ambayo yanawezesha wabunifu kuleta bunifu zao mbalimbali na kuzitangaza ili kuwawezesha kulifikia soko.

Akizungumzia kuhusu ubunifu wake alisema kifaa alichobuni kina uwezo wa kupima kiasi cha gesi kilichoko kwenye mtungi ili kumwezesha mtumiaji kujua ujazo sahihi.

"Kifaa hichi pia kinamwezesha mtumiaji kujua kiasi kilichobaki kwenye mtungi ili kuondokana na tatizo la gesi kukatika bila mtumiaji kuwa na taarifa hivyo kupitia kifaa hicho mtumiaji atajua gesi yake inaisha lini na kiasi gani kimebaki.

"Pia kifaa hichi kina mfumo ambao unaweza kumuunganisha mtumiaji gesi na msambazaji ili mara gesi inapoisha kuna kitufe mtumiaji anabonyeza ambacho kinatuma taarifa kwa msambazaji kuonyesha aina ya mtungi, kiasi, eneo la mteja ili aweze kupelekewa huduma hiyo," alisema Joasi.

Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU), huku wabunifu zaidi ya 480 wakisajisajiliwa kwa ajili ya kushiriki mashindano hayo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Aldof Mkenda, alisema mashindano hayo kitaifa yamepangwa kufanyika jijini Dodoma kuanzia Mei 15 hadi 20, mwaka huu kwa kushirikisha wabunifu kutoka sehemu mbalimbali.

Alisema mashindano hayo ni sehemu ya mikakati ya serikali ya awamu ya sita ya kuongeza hamasa ya matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kama nyenzo ya kutatua kero za kiuchumi na kijamii.

"Mashindano haya ni muhimu sana ndio maana serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuendeleza mashindano hayo katika Wiki ya Ubunifu iliyoandaliwa kwa kushirikiana na programu ya FUNGUO ya UNDP inatarajiwa kufanyika katika mikoa 17 nchini ambayo ni Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Iringa, Mwanza, Zanzibar, Tanga, Kilimanjaro, Morogoro, Njombe, Kagera, Mtwara, Kigoma, Mara na Ruvuma.

Aidha, Prof. Mkenda alisema, kupitia MAKISATU ya mwaka 2019, 2020 na 2021, wizara imefanikiwa kuibua na kutambua wabunifu wachanga 1,785 na kupitia wabunifu hao, bunifu 466 zilikidhi vigezo na zimetambuliwa na kuhakikiwa.

"Kati ya hizo bunifu mahiri 200 tayari zinaendelezwa na serikali ili kufikia hatua ya kubiasharishwa na kati ya bunifu zinazoendelezwa na serikali, 26 zimeshafikia hatua ya kubiasharishwa, huku 95 zikiwa katika hatua ya sampuli kifani na nyingine zipo katika hatua za awali za kuandaa sampuli kifani," alisema.




Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amos Nungu, akizungumza na wabunifu kuhusu umuhimu wa bunifu zao kutambuliwa na serikali, katika Wiki ya Ubunifu inayoenda sambamba na mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU), jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Ummy aagiza fedha za polio zitumike sahihi

Na Renatha Msungu, DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameziagiza halmashauri na mikoa nchini, kuhakikisha fedha zilizotolewa kwa ajili ya kampeni ya ugonjwa wa polio zinatumika kwa matumizi sahihi huku akisisitiza elimu itolewe kwa jamii ili kuepuka upotoshaji wa chanjo ya ugonjwa huo.

Mwalimu alisema hayo jana jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kitaifa ya utoaji chanjo ya ugonjwa wa polio kwa watoto kuanzia mwaka sifuri hadi mitano.

Waziri huyo alisema hakuna sababu ya halmashauri hizo kubadilisha matumizi ya fedha hizo kinachotakiwa zielekezwe katika utoaji chanjo ili kusaidia kuwakinga watoto na ugonjwa wa polio. Alifafanua kuwa ugonjwa wa polio hauna tiba, lakini kinga ipo hivyo wazazi na walezi wanapaswa kuwapeleka watoto kwa ajili ya kupata chanjo hiyo ambayo inamsaidia mtoto kutopata akiwa na umri chini ya miaka mitano.

"Baada ya uzinduzi huu naomba mkatekeleze majukumu ya utoaji chanjo katika zahanati, vituo vya afya, kwa njia tembezi, mkoba pamoja na kupita nyumba kwa nyumba," alisema Mwalimu.

Akizungumzia utoaji elimu kwa jamii, aliwataka viongozi katika halmashauri mbalimbali kutoa elimu kwa jamii ili kuepusha upotoshaji chanjo ya polio na nyingine zinaleta madhara kwa watoto.

"Nawaomba Mkurugenzi wa Afya TAMISEMI katika hili la elimu mkasimamie, hakikisheni wenyeviti wa vijiji pamoja na viongozi wa serikali za mitaa wanatoa elimu kwa wananchi ya upataji chanjo badala ya kupotoshana," alisema Mwalimu.

Kadhalika, alisema baada ya uzinduzi huo wanatarajia kutoa chanjo katika mikoa 21 ya Tanzania na wanatarajia kuwachanja watoto 10,295,316 ambao wanalengwa kuchanjwa katika zoezi hilo.

"Zoezi la utoaji chanjo hiyo litakuwa la siku nne kwa nchi nzima na huduma zitatolewa katika vituo vya kutoa huduma za afya, ikiwamo zahanati, vituo vya afya, hospitali lakini kutokana na kufahamu wazazi wanashughuli zao hivyo zoezi hilo litafanyika kwa njia tembezi na mkoba ikiwamo kuwafuata maeneo watoto walipo ili kuwakinga," alisema Mwalimu.

Alisema zoezi hilo pia linafanyika visiwani Zanzibar na wanalenga kuchanja watoto 281,489 na jumla bara na visiwani wanatarajia kuchanja watoto 10,500,000, na kuwataka wazazi viongozi wa serikali za mitaa na vitongozi kutoa ushirikiano ili watoto wapate chanjo.

Alitoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa polio kwa kuwapeleka watoto kupata chanjo ya ugonjwa huo nchi nzima pamoja na magonjwa mengine. Alisema serikali itaendelea kuchukua hatua zote stahiki dhidi ya ugonjwa huo, ikiwamo kufanya tathmini ya hatari ya ugonjwa wa polio katika mikoa yote ya Tanzania Bara na visiwani ikiwamo kuimarisha utoaji chanjo kwa watoto wote wanaohisiwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Aliwataka wataalamu wa afya kuimarisha huduma za utoaji wa chanjo kwa kipindi chote cha kampeni na baada ya kwamba serikali haijasimamisha utoaji wa chanjo nyingine kwa sababu watoto bado wanazaliwa.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, alisema wamepokea dozi 551,209 na wanatarajia kuwafikia watoto 479,156 katika halmashauri zote nane.



# Wakulima wa kahawa wawezeshwa miche

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIKA kuhakikisha wakulima wa kahawa Nyanda za juu kusini Kanda ya Mbeya, wanapata mbegu za uhakika na zenye ubora, Taasisi ya Utafiti wa zao hilo Tanzania (TaCri) imepanga kuzalisha miche 20,000 kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wakulima.

Kwa mujibu wa Meneja wa Utafiti zao la Kahawa Tanzania wa TaCri Nyanda za Juu Kusini Kanda ya Mbeya, Dismas Pangalasi, uzalishaji wa miche hiyo utaanza katika msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2022.

Alisema licha ya serikali kuagiza taasisi hiyo kuzalisha miche ya mbegu 20000 kwa msimu ujao wa kilimo lakini wao pia wameweka malengo yao ili kuhakikisha wakulima wanapewa mbinu bora za kuongeza uzalishaji.

Alisema miongoni mwa mambo waliyofanikiwa ni pamoja na kugundua aina bora 19 za kahawa aina ya Rabika zenye ukinzani na magonjwa ikiwamo ya kutu katika mimea ya majani.

Alisema aina hizo za mbegu zikiwamo na teknolojia za kutumia kwenye kilimo zimewasaidia wakulima kupata mavuno mengi na kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

Aliongeza kuwa kwa mwaka 2020 /2021 walizalisha miche milioni tatu na kuweza kuzisambaza kwa wakulima licha ya kuwa mahitaji yalikuwa ni miche takribani milioni 18 kwenye Kanda ya Mbeya hali inayoonesha uhitaji wa miche hiyo kuwa mkubwa.

Alidai kuwa jumla ya wakulima 77,000 wanalima zao hilo huku hekta 58,500 zikilimwa na kuzalisha wastani wa tani 18,000 hadi 19,000 kwa mwaka katika kanda ya Mbeya.

Aidha alisema miongoni mwa mipango katika kukuza sekta ya kilimo cha kahawa nchini taasisi hiyo imepanga kuzalisha miche tani 30,000 katika kipindi cha miaka mitano ijayo kwa kuzingatia ubora na uwezo wa mkulima kupata mavuno mengi. Licha ya uzalishaji wa miche hiyo pia watahakikisha wanazingatia uwezo wa kukinzana na magonjwa mbalimbali ambayo yanashambulia mimea ya zao hilo la kahawa.

"Licha ya mikakati ya taasisi hii, kuwasaidia wakulima lakini bado tunakabiliwa na mahitaji makubwa ya miche ya kisasa kwa wakulima ukilinganisha na uzalishaji wenyewe ambapo kwa sasa ni tani milioni tatu na mahitaji yakiwa ni milioni 18 kwa Kanda ya Mbeya," alisema Pangalasi.

Aidha kuna tatizo la baadhi ya wakulima na wadau kutokujua umuhimu wa kufanya utafiti wa afya ya udongo licha ya kupeleka miche kwa wakulima hivyo kuchangia mavuno kutokuwa bora na mengi.

Kutokana na hali hiyo, alitoa hamasa wakulima pamoja na wadau wengine wanaohusika na mnyororo wa thamani wa zao la kahawa kuhamasishana kupima afya ya udongo ili kujua mbegu gani inapaswa kutumika katika kulingana na kila eneo.

Kwa upande wake, Meneja wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Cafe Africa Tanzania, Dafrosa Sanga alisema miongoni mwa majukumu ya shirika hilo ni kuwahamasisha wakulima upandaji wa miche bora ya kahawa ili kupata mavuno mengi.

Alisema katika jukwaa la wakulima pamoja na wadau wanaohusika kwenye mnyororo wa thamani wa zao la kahawa, kunatoa fursa ya kujadili kwa pamoja namna ambayo itasaidia kukidhi mahitaji ya miche kwa wakulima ili waongeze uzalishaji na kulima mimea ambayo itatoa mavuno bora ambayo yatakidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Dk. Nadhifa Kemikimba, akionyesha kitabu kilichoainisha mpango jumuishi wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji Bonde la Ziwa Rukwa, iliyoandaliwa mwaka 2020 kwa lengo la kutunza na kuendeleza rasilimali mbalimbali zinazopatikana kwenye ziwa hilo kwa wadau, wataalamu na wasimamizi wa jumuiya za watumia maji kutoka Mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi, wakati wa jukwaa la wadau wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Athari za mabadiliko tabianchi zaleta shida

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MABADILIKO ya tabianchi yametajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa chakula na wadudu wachavushaji ambao ni muhimu kuchangia uzalishaji wa mazao pamoja na kuboresha afya ya mazingira.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Idara ya Utafiti na Machapisho wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Dk. Fredrick Ojija wakati wa uwasilishwaji wa tafiti anazofanya katika Chuo hicho kwa wananchi na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Stela Farm iliyopo Iwambi jijini Mbeya.

Dk. Ojija alisema kuwa wadudu wachavushaji ni muhimu kwa ajili ya afya ya udongo na urutubishaji wa mazao lakini kuna idadi kubwa ya wananchi ambao hawafahamu umuhimu huo hivyo kupata mavuno hafifu. "Chuo chetu tumekuwa tukifanya tafiti mbalimbali lengo ni kusaidia wananchi hususani wakulima kulima kwa tija na kuvuna mazao mengi. Hivi karibuni tumeshuhudia mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo yanaweza kusababisha madhara makubwa ya kupungua kwa chakula pamoja na kupungua kwa wadudu wachavushaji ambao ni muhimu kwa sababu huchangia katika uzalishaji mazao ya chakula," alisema Dk. Ojija.

Aidha alibainisha kuwa Chuo kimekuwa kikitoa fedha kwa watafiti wake ili wafanye tafiti kwa lengo la kusaidia jamii na kutoa elimu kwa wanafunzi, pia kuongeza uelewa kwa wananchi juu ya wadudu wachavushaji.

Aidha Mhadhiri huyo amesema kuwa kwa sababu wananchi hawajui namna ya kuwahifadhi wadudu hao wameandaa utaratibu wa kuwafikia wananchi kuwapatia elimu kupitia mradi huo kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira.

Mkuu wa Idara ya Sayansi Asilia, Dk. Eliezer Mwakalapa alisema chuo hicho kimekuwa kikiwasaidia kufanya tafiti mbalimbali ambazo zinawasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

# Wahujumu wa miundombinu Bonde Ziwa Rukwa kukiona

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Dk. Nadhifa Kemikimba, amewaagiza viongozi wa Bonde la Maji la Ziwa Rukwa, kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaobainika kuiba miundombinu iliyojengwa katika bonde ili iwe fundisho kwa watu wengine.

Dk. Kemikimba alifikia uamuzi huo baada ya kupokea taarifa juu ya wimbi la wizi wa bakodi zilizojengwa kwenye mito ambayo inapeleka maji kwenye ziwa Rukwa.

Alisema serikali ilitoa fedha kwa ajili ya kujenga bakodi hizo kwa lengo la kuweka mipaka kwenye mito na ziwa ili kuzuia shughuli za kibinadamu zisiendelee ndani ya maeneo hayo.

"Nimesikia hapa baadhi yenu mnalalamika kwamba kuna wizi wa bakodi unaofanywa na baadhi ya wananchi ambao tunawaita wahujumu uchumi, natoa agizo wote wakamatwe kwa sababu mnawafahamu lakini mnaendelea kuwalea," alisema Dk. Kemikimba.

Aidha Dk. Kemikimba alizikumbusha jumuiya za watumia maji kuhakikisha wanaendelea kuwa mabalozi wazuri katika utunzaji wa miundombinu ya maji ili kulinda usalama wa mimea, viumbe hai vilivyoko ndani ya vyanzo vya maji ambavyo vinapeleka maji ndani ya Ziwa Rukwa.

Alisema kuna suala la shughuli za kibinadamu kama vile uchimbaji wa madini katika Wilaya ya Chunya na Wilaya ya Songwe, hivyo ni muhimu vyanzo vya maji kuzunguka shughuli hizo vikatunzwa ili kulinda afya za watumiaji maji.

Aliwaomba wamiliki wa machimbo na wachimbaji kutoharibu vyanzo vya maji licha ya shughuli hizo kuhitaji maji mengi katika kuzalisha dhahabu lakini ni muhimu wakazingatia suala la utunzaji mazingira ikiwamo vyanzo vya maji.

"Hatuwezi tukazuia shughuli za kibinadamu kufanyika kwa sababu tunaishi kwa kutegemeana jambo la muhimu ni nyie wataalam kuangalia namna bora mtaweza kuwadhibiti wale wote ambao wataingia kwenye vyanzo vya maji, hili ndio jambo la msingi lakini mtoe elimu kwanza kabla ya kuanza kuwafukuza ni muhimu ili wajue itasaidia," alisema Dk.Kemikimba.

Mhandisi wa Umwagiliaji, Mkoa wa Rukwa, Lucas Athanas alisema wanaendelea na jitihada mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ikiwamo kuanzisha skimu mbalimbali za umwagiliaji kwenye mazao kama vile mpunga na mahindi ili kuzuia uvamizi kwenye vyanzo vya maji.

Alisema hadi sasa zaidi ya skimu tano zinajengwa kwa lengo la kukabiliana na tatizo la wakulima kuvamia vyanzo vya maji kwa ajili ya shughuli za kilimo.



## Wanafunzi 11,700 warejeshwa shuleni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema imefanikiwa kuwarudisha shuleni wanafunzi 11,735 waliotoroka na kujiingiza katika ajira.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Ali Abdulgulam Hussein, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu hatua za utekelezaji wa mradi wa kuwarudisha shuleni wanafunzi waliotoroka.

Alisema mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Qatar kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na umepata mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka miwili cha utekelezaji wake.

Watoto wenye umri wa miaka saba hadi 14, alisema wamerudishwa shuleni baada ya ushirikiano mzuri kati ya viongozi wa shehia, wazazi na kamati za shule.

Alisema kwa upande wa Unguja, wanafunzi 3,073 wamerudishwa na kuanza masomo yao, wakati kwa Pemba ni watoto 6,662.

Naibu Waziri alisema wanafunzi wengi wanatoroka shule na kujiingiza katika ajira ngumu zikiwamo za kuvua baharini na kugonga kokoto, hivyo kuhatarisha maisha yao.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaendelea kutekeleza mradi wa kuwarudisha shuleni watoto waliotoroka na kujiingiza katika ajira mbaya zinazohatarisha maisha yao. Ili kufanikisha hili, tunawaomba wazazi kutoa ushirikiano," alisema.

Maeneo ya ukanda wa fukwe za bahari unatajwa kuongoza kwa watoto kutoroka shule na kujiingiza katika ajira ngumu ikiwamo kutembeza watalii pamoja na kuvua baharini.

# Rais Samia apongezwa kuitangaza nchi kimataifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuitangaza Tanzania katika utalii kupitia filamu ya Royal Tour hatua ambayo wamesema itaimarisha na kukuza sekta hiyo.

Wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, wawakilishi hao walisema hatua hiyo ni ya kujivunia na itaifanya Tanzania kupata mafanikio makubwa kupitia utalii.

Mwakilishi wa Bububu, Hussein Ibrahim Makungu, alisema Rais Samia anastahili kupongezwa kutokana na kuwa Rais wa kwanza kushiriki katika filamu kutangaza vivutio vya Tanzania.

Alisema matarajio makubwa kwa wananchi wa Tanzania ni kupokea idadi kubwa ya watalii watakaotembelea nchini kutokana na matokeo ya filamu hiyo ambayo imefungua milango ya fursa za uwekezaji.

"Nachukuwa nafasi hii kumpongeza kwa dhati Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ya kutangaza utalii wa Tanzania kwa kushiriki katika filamu ya Royal Tour ambayo imefungua fursa za utalii duniani," alisema.

Mwakilishi wa Viti Maalumu mkoa wa Kaskazini Pemba, Bihindi Hamad, alimpongeza Rais Samia kwa kushirikiana na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kutumia fursa ya kuvitangaza vivutio vya utalii katika ramani ya kimataifa.

"Mheshimiwa Spika, Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha njia kufungua milango ya fursa ya utalii nchini. Lakini serikali nayo inatakiwa kuchukua juhudi za kujenga mazingira mazuri kwa kuimarisha miundombinu ya barabara zitakazowafikisha katika maeneo hayo," alisema.

Mwakilishi wa Ziwani, Suleiman Makame, alieleza kufurahishwa na filamu ya Royal Tour kwa kazi kubwa ya kutangaza vivutio vya utalii ikiwamo kulinda utamaduni wa wananchi wa Zanzibar pamoja na mila na silka zake.

"Filamu ya Royal Tour nimeiona mwenyewe ambayo imetangaza kwa kiwango kikubwa utamaduni wa watu wa Zanzibar wenye kulinda mila na silka pamoja na vivutio vya kale vya miji ya kihistoria," alisema.



Mwakilishi wa Viti Maalum, Salha Muhammed Mwinjuma, akichangia hoja katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yasema maeneo ya uwekezaji hayajatelekezwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema maeneo huru ya kiuchumi na uwekezaji yaliyoko Micheweni Pemba na Fumba Wilaya ya Mjini Unguja hayajatelekezwa.

Badala yake imesema inaendelea na mikakati ya kuwatafuta wawekezaji kuwekeza pamoja na kuweka miundombinu ikiwamo ujenzi wa barabara.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema hayo jana wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23 katika kikao cha baraza hilo.

Alisema mikakati ya serikali ni kuhamasisha wawekezaji zaidi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya aina mbalimbali ambavyo vitasaidia kuzalisha ajira kwa wananchi.

Waziri Omar alisema maeneo huru ya kiuchumi yalianzishwa katika mwaka 1992 ambayo lengo lake kuwavutia wawekezaji kutumia fursa ya kuwekeza katika miradi ya viwanda kwa uzalishaji na kusafirisha nje ya nchi.Alisema maeneo huru ya Fumba yanaendelea kutumiwa na wawekezaji mbalimbali Unguja na Pemba na kwamba iko miradi inayotekelezwa ikiwamo uwekezaji wa kiwanda cha maziwa na vinywaji.

"Mheshimiwa Spika maeneo huru ya Fumba yanaendelea kutumika vizuri katika uwekezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa viwanda vya kuzalisha maziwa na vinywaji," alisema.

Kuhusu maeneo huru yaliopo Micheweni mkoa wa Kaskazini Pemba, Omar alisema juhudi za kulitangaza eneo hilo pamoja na kuweka miundombinu muhimu zinaendelea ikiwa ni hatua za kuwavutia wawekezaji.

Alitaja eneo hilo tayari miundombinu muhimu imefanikiwa kufikishwa ikiwamo ya majisafi na salama, umeme pamoja na ujenzi wa barabara.

Waziri alisema ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 22 ya Chake Chake hadi Wete unatarajiwa kutekelezwa na kukamilika kwake kutaiunganisha mikoa miwili ya Pemba katika uwekezaji. "Hiyo ndiyo mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuyaendeleza maeneo huru ya kiuchumi yaliyoko Micheweni Pemba pamoja na Fumba Unguja. Tumefikisha miundombinu na sasa kazi yetu kuyatangaza kimataifa zaidi," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**George Marwa Migera**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya Nissan Vannette yenye namba za usajili **T.455 CAQ** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na George Marwa Migera kwa simu namba **0785670077**

POLISI TAARIFA/
**SHI/SHI/RB/78818/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LIMITED**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BAJAJ BOXER** yenye usajili namba **MC420 BJZ,** CHASSIS NAMBA **MD2A21BZ1GWC85909,** ENGINE NAMBA: **PFZWGC30022.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**KW/RB/2072/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ZAINAB MPUYIKI MGUDE**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya Honda yenye usajili namba **MC359 BUU,** CHASSIS **NAMBA MD201000342.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**KW/RB/2072/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE



**MAY C MILLANZI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index no **S.2153-0024** kilichotolewa na baraza la Mitihani kupitia shule ya Sekondari Aquinas Sekondari Mwaka 2009 Mkoa wa Mtwara, Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi. **MTW/MTW/RB/358878/2021.**

## TEGEMEZA AUCTION MART LIMITED

P.O. Box 77395 – DAR ES SALAAM.

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**Kesi namba 117/2021**
**Mdai: ELIZABETH NGOMA**
**Mdaiwa: FELIX MODEST**

Kwa Mamlaka tuliyopewa na Hakimu Mfawidhi Mahakama ya Mwanzo Kimara kutakuwa na mnada wa hadhara wa uuzaji wa nyumba nzuri ya kisasa.

| ENEO LA MNADA | AINA YA MALI | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|
| Goba, Tegeta kituo cha Darajani Dar es salaam | Nyumba ya kisasa | 21/5/2022 muda ni saa 4:00 asubuhi. |

**TARATIBU ZA MNADA**

1. Mali itauzwa kama ilivyo
2. Gharama za kubadili umiliki ni za mteja
3. Unalipa 25% baada ya siku 14 unamalizia 75%. Usipofanya hivyo baada ya siku 14 pesa haitarudishwa iliyotolewa awali.

**Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba 0719 187 677.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALEXANDER A. ANGELO**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 444 AKC.** yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/197342/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI/TARAKA/MIRATHI NAMBA: 216....2018**

**MUOMBAJI: MARIAM MOHAAMED YUSUPH**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: MAGRETH LEONARD MKUMBI DAR ES SALAAM**

**Kwa: MAGRETH LEONARD MKUMBI**

**Ombi la msimamizii: MAGRETH LEONARD MKUMBI**
**Madai ya : KUFUNGA MIRATHI NO 216/2018**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikiliwa mnamo tarehe 08 mwezi 06 mwaka 2022 saa2:30 asubuhi.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 10 mwezi 05 mwaka 2022.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU ISACK SAMWEL BUJANJA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T585AVQ** aina ya ISUZU Rangi Dark Nyeupe yenye Chassis No. **NKR58L-7106008,** Engine **No.4BC2-801526** yenye jina la NJUNWA PONTIANANGELO KAENA Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba
**DOD/DOD/RB/184868/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA - KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI NA. 117/2019**

**MALIKI SUDI ..............................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**BUKOBA MUNICIPAL COUNCIL NA WENZAKE........WAJIBU MAOMBI**

**KWA:** ABDALLAH KAMUGISHA, TUMAINI MUTAZAMBA, JAPHES NOAH, SIMON PAUL, ZITA MKUBULO, SUDI BI SALUMU, JESSE MUGISHA, GERALDINA KAHAGAMA, AUSON JUSTIAN, STEWATH SHUMBUSHO, LUCIA GERUMAN, HAWA KICHWABUTA, ALISTIDIA FRANCIS, SIRI GERASHOP, MAMA ALIRA, LILIAN ALBERT RUGANGILA,
LONGINO LUBULI, EDSON MUSOKE, OSSEA YUSTASI, AUTUSONI KAJWAHU, BADRU BADRU, KALIKAWE, JULIANA NDIBALE, GODFREY, ALFRED, KANISA, TRESIUS THOMAS, JAPHES NOAH, ADOLF BANYENZA, KHALID KHAMIS, PONTIAN RUTASHOBYA (POPOTE PALE MLIPO)

Mnaarifiwa kuwa Maombi Na. 117/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 06/06/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi. Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria nyinyi wenyewe/ mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa. Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 12/05/2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**

**Kituo cha NYANKUMBU**

**Shauri a madai/Ndoa Na 75/2022**

**Jina la Mdai: SAID EVARIST MATUMBA**

**Jina la Mdaiwa: HAMIMU KAHAMBA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: HAMIMU KAHAMBA**
**WA MTAA WA MSETO-GEITA**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai:Unaamriwa na Mahakama hii ufike bila kukosa au kuchelewa ili kujibu madai dhiki yako ya Tsh. 2,665,000/-**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katikaMahakama hii Tarehe 23 Mwezi 05 Mwaka 2022 saa 2.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo..
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 17 Mwezi 05Mwaka 2022

RESIDENT MAGISTRATE
GEITA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO MWAMBAO**

**SHAURI LA MIRATHI**

**IBRAHIM MARIJANI GAMA...............MSIMAMIZI**

**DHIDI YA**

**SALMA MBARAKA AWADHI............MAREHEMU**

Kwa mdaiwa MBARAKA MTEI , popote ulipo unatkiwa kuhudhuria mahakamani bila ya kukosa tarehe 27/05/2022, saa 2:30 asubuhi, kujibu madai yako, tambua kuwa kutokufika kwako shaurini mahakama itasikiliza shauri upande mmoja na maamuzi yatatolewa

Imetolewa leo tarehe 16/05/2022

HAKIMU MFAWIDHI,
MAHAKAMA YA MWANZO MWAMBAO,
BAGAMOYO.

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

HABARI KITAIFA

# Wakulima wadogo 20,000 wapata fursa

**Na Mwandishi Wetu**

MATUNDA ya kampeni ya kilimo ni biashara iliyozinduliwa Aprili mwaka huu na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe yameanza kuonekana baada ya kampuni ya Silverlands Tanzania kutoa fursa zaidi ya 29,000 kwa wakulima wadogo wa kitanzania kupitia biashara ya ufugaji wa kuku.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na ofisa masoko wa kampuni hiyo, Mwanamvua Ngocho, wamedhamiria kuchochea mafanikio katika kuimarisha sekta ya kilimo cha ufugaji nchini.

Alisema malengo yao ni kuhakikisha wanamkomboa mkulima mdogo kupitia kilimo biashara cha kuku sambamba na ajenda ya serikali ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini kufikia mwaka 2030.

"Kampuni yetu inajivunia kuwa miongoni mwa wadau wa sekta ya kilimo nchini baada ya kuwanufaisha zaidi ya wafugaji 29,000 wa kuku nchini, na hawa sio kuku wa kawaida, ni zao la kisasa liitwalo Sasso ambao wanakua kwa haraka, katika miezi miwili na nusu wanafika kilo mbili, wanahimili magonjwa tofauti na aina nyingine ya kuku," alisema Mwanamvua.



"Pia tumejikita katika utoaji wa elimu kwa wakulima kupitia chuo kilichoko mkoani Iringa, biashara ya kuku, kuzalisha vyakula na vifaranga, kutoka mwaka 2014 mpaka sasa kampuni imekuwa yenye uzalishaji mkubwa wa vyakula vya kuku na ni ya tatu kwa uzalishaji wa vifaranga," alisema Mwanamvua.

Aliongeza kuwa kuku na chakula kinachozalishwa na Silverlands Tanzania kinawalenga wafugaji wadogo ambao huwakilisha kundi kubwa la wafugaji kusini mwa jangwa la Sahara ambapo kwa asilimia 60 wana kipato duni huku wengi wao wakilima mahindi ambayo yamekuwa chachu ya ukuaji wa biashara ya kuku nchini.

Vile vile alibainisha kuwa uzalishaji wa kuku na mayai umesaidia kupunguza utapiamlo kwa watoto, ambapo kwa mujibu wa tafiti zinaonyesha kuwa licha ya Tanzania kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 120, lakini asilimia 35 ya Watanzania bado wana utapiamlo.

Kampuni hiyo kwa sasa inanunua mahindi na soya kutoka kwa wakulima wadogo 29,000, inaendesha vituo 19 vya usambazaji nchini kote vikiwa na wasambazaji wadogo zaidi ya 350 wanaouza bidhaa zake kwa wafugaji wadogo wa kuku 134,000, huku asilimia 75 kati yao wakiwa ni wanawake.

**Alisema malengo yao ni kuhakikisha wanamkomboa mkulima mdogo kupitia kilimo biashara cha kuku sambamba na ajenda ya serikali ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini kufikia mwaka 2030.**


**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI YA SIKU 14/MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA (BOA)** tunatoa Notisi ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa mdaiwa tajwa hapo chini kwenye jeduari alipe deni analo daiwa na benki hiyo Pamoja na riba.kushindwa kufanya hivyo mali iliyowekwa kama dhamana itauzwa kwa njia ya mnada wa Hadhara kufidia deni hilo.Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo tarehe na muda kama inavyoonyeshwa kwenye jeduari hapo chiniinavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|
| 1. | MKASI AGRI PRODUCTS SUPPLIES LIMITED / BARAKA NSAJIGWA KYEJO | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA. P 5469 ENEO LA UBUNGO MANISPAA YA UBUNGO· | 04.06.2022, JUMAMOSI SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHART YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/766-309913**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**BANK OF AFRICA PLC**
**P. O. BOX 3054 DAR ES SALAAM**



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA UTAMADUNI WA USALAMA MAHALA PA KAZI KWA EACOP LTD KWA TANZANIA**
**KUMBUKUMBU NO: 10007720**

Kampuni ya EACOP Ltd inahitaji huduma kutoka kwa wakandarasi wazoefu na wanaoheshimika kuwezesha utayarishaji wa mpango wa utamaduni wa usalama mahala pa kazi kwa kampuni na mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) nchini Tanzania.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 296 ziko Uganda na 1,147 ziko Tanzania.

Miundo mbinu itakayojengwa juu ya ardhi kwa Tanzania itahusisha vituo 4 vya pampu, vituo 2 vya kupunguzia kasi ya mtiririko wa mafuta; kituo kikuu cha kuhifadhia mafuta karibu na bahari (Marine Storage Tank) na kituo cha kupakilia mafuta (Load Out Facility); kambi 12 za wafanyakazi na za kuhifadhia mabomba, barabara za kuelekea kwenye vituo na makambi; na vituo vya kuvunia mwanga wa jua (solar farms). Miundo mbinu itakayojengwa juu ya ardhi kwa Uganda itahusisha vituo 2 vya pampu; kambi 4 za wafanyakazi na za kuhifadhia mabomba, barabara za kuelekea kwenye vituo na makambi.

EACOP Ltd ilianzishwa tarehe 15 Februari 2022 na hatimaye itahusisha hadi watu 6,000 kutoka kwa wakandarasi na wakandarasi wasaidizi kutoka katika mataifa na tamaduni mbalimbali, yaliyosambaa kutoka sehemu mbalimbali za kijiogorafia.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Dhamira ya kampuni ni kuhakikisha usalama mahala pa kazi wa watu na mali, kuhifadhi maliasili na kulinda mazingira halisi na ya kibinadamu kwa kushirikiana na wenyeji huku ukidumisha utiifu wa kanuni zote zinazotumika na vibali vinavyotolewa na wadhibiti. Lengo la kampuni ni kutokuwa na madhara kwa watu, mazingira, kwenye jamii inapofanyia kazi, na mali zake na kwa sifa ya kampuni. Kampuni kwa sasa inaanzisha mifumo yake ya usimamizi, michakato na ingependa kuunda utamaduni wa kiwango cha kimataifa wa afya, usalama mahala pa kazi na mazingira (HSE).

EACOP inahitaji huduma za makampuni au mashirika yenye uzoefu na yenye sifa nzuri ili kusaidia EACOP Ltd kuandaa mpango bora wa utamaduni wa usalama mahala pa kazi kwa kampuni na mradi wa EACOP Ltd. Lengo litakuwa kwa EACOP na wakandarasi wao kuendeleza utamaduni dhabiti wa usalama katika mradi wote kwa kutumia lugha moja na zana kwa pamoja na wakandarasi.

Vigezo muhimu ambavyo vitazingatiwa katika uchaguzi wa program ya utamaduni wa usalama inayopendelewa itajumuishwa:

- Progamu inayowezesha tamaduni dhabiti ya usalama mahala pa kazi ambayo itaongeza ushiriki wa wafanyakazi, na utashughulikia usalama mahala pa kazi, mazingira, jamii, ubora na ufanisi wa kazi.
- Programu ambayo inajenga mawazo ya 'kufahamu hatari' ili kuwaweka wafanyakazi na familia zao salama kazini, nyumbani na barabarani.
- Programu ambayo inafaa kwa wafanyakazi wengi na wa tamaduni mbalimbali ambao wana uelewa mdogo sana wa hatari na utamaduni mdogo wa usalama mahala pa kazi.
- Programu ambayo ni rahisi, inayonyumbulika na ya haraka kutekelezwa (ndani ya miezi si miaka)
- Programu inayofaa kwa miradi mikubwa na/au mashirika yanayo anza kufanya kazi.
- Programu inayoweza kufasiliwa kwa ajili ya EACOP na hatari pamoja na changamoto za miradi.
- Programu yenye rekodi bora na utekelezaji wa HSE (miradi mikubwa ya kimataifa).
- Uzoefu na uwezo wa washauri maalumu/wakufunzi walio pendekezwa kwa EACOP.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au mashirika yatakayo onyesha nia yanatakiwa kuwa na vielelezo vifuatavyo:

- Uzoefu/utendaji katika kutoa programu sawa za utamaduni wa usalama zilizoainishwa hapo juu kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania/Uganda, au kwa angalau uzoefu na utendaji bora wa miaka 10 kwa huduma inayofanana na hiyo kimataifa
- Wafanyakazi waliofuzu na wenye uzoefu wa kutekeleza program za utamaduni wa HSE kwa miradi mikubwa ya gesi na mafuta.
- Uzoefu wa kutengeneza programu za kitamaduni za HSE ambazo hutoa utendakazi wa kiwango cha kimataifa cha HSE
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na uwasilishaji wa akaunti za fedha za muda wa miaka mitatu iliyopita
- Muonesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia yake ni muhimu sana
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani
- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Ubora, Afya, Usalama mahala pa kazi na Mazingira, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani ya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa leseni unaofaa kutoka kwa mamalka husika ndani ya nchi kwa ajili ya huduma
- Uthibitisho wa kusajiliwa na mamlaka ya mapato Tanzania na cheti kinachoonyesha uthibitisho ulipaji wa kodi kwa mwaka wa hivi karibuni.

Makampuni yenye nia ya kuleta maombi na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **procurement.tz@eacop.com** saa au kabla ya saa **10 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **31 Mei 2022.** Ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb.** Taarifa zote ziwasilishwe kwa lugha ya Kingereza

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Makampuni ya awali yenye vigezo ndiyo yatakayopokea mrejesho. Taasisi zitakazokidhi vigezo ndizo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

216865001



Kikosi cha Espanyola ambacho kimefanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi ya Soka ya Mchangani (Betika Sodo Bingwa wa Ligi) msimu huu katika kituo cha Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BOCCO AFUNGUKA BAADA KUPACHIKA BAO CHAMAZI

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Simba, John Bocco ameonyesha furaha yake kufunga bao kwenye Uwanja wa Azam Complex, ambao ameuzoea kutokana na kuuchezea kwa muda mrefu.

Akizungumza juzi usiku baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania kati ya timu hiyo dhidi ya Azam FC, straika huyo amesema ni jambo la furaha na la kujivunia kufunga bao kwenye uwanja huo baada ya muda mrefu.

Bocco alifunga bao dakika 44 kwa kichwa kufuatia mpira wa faulo uliopigwa na mchezaji mwenzake wa zamani wa Azam, Shomari Kapombe, baada ya yeye mwenyewe kuangushwa nje kidogo ya eneo la hatari na Sospeter Bajana.

Lilikuwa ni bao la kusawazisha baada ya Rodgers Kola kuitanguliza Azam FC katika mechi iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1.

"Nimefurahi sana kufunga bao tena kwenye uwanja huu ambao nimeuzoea, ambao ilikuwa ni mwanzoni tu mwa 'karia' yangu ya soka, nimekuja tena hapa baada ya muda mrefu, nimebahatika kufunga," alisema Bocco ambaye alijiunga na Simba akitokea Azam mwaka 2017 ambayo nayo ilimsajili kutoka Cosmopolitan 2007.

"Tunaendelea kupambana, msimu haujaisha, ila haujaenda vizuri, tunaendelea kupambana ili tuumalize vizuri, bado tuko kwenye mbio, unaweza kukawa siyo bora kama misimu mingine, lakini ni lazima tumalize tukiwa na ubora fulani mzuri hivi," alisema Bocco.

Pamoja na kuonekana kama wanauachia ubingwa kwa watani zao, Yanga, nahodha huyo alisema bado wanapambana kwenye ligi hiyo na mashindano ya Kombe la FA ili wasitoke kapa msimu huu.

"Kombe la FA lipo mikononi mwetu, ni uamuzi wetu kulibakisha au kulipoteza liende sehemu nyingine," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (katikati), akiwa ameshika jezi maalum ya Mashindano ya NBC Dodoma Marathon yatakayofanyika Juni mwishoni mwaka huu, wakati wa uzinduzi wa mbio hizo jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Rais wa Chama cha Riadha Tanzania (RT), Silas Isangi, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage, Mkurugenzi Mtendaji Makampuni ya Bima ya Sanlam, Julius Magabe na Mkurugenzi Mkuu wa Efm Radio na TV, Dennis Busulwa (Ssebo). **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Espanyola wababe Betika Sodo

**Mwandishi Wetu**

TIMU ya Espanyola imeibuka mabingwa wa Ligi ya Soka ya Mchangani maarufu Betika Sodo Bingwa Ligi baada ya Jaga kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Care Boys katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Kituo cha Dar es Salaam.

Katika ligi hiyo inayodhaminiwa na kampuni ya michezo ya kubashiri ya Betika, Espanyola ilijihakikishia ubingwa ikiwa imetoka kuchapwa bao 1-0 na Hard Numbers kwenye uwanja wa Msisiri Kinondoni.

Matokeo hayo yaliifanya Espanyola kutwaa ubingwa huo baada ya kufikisha pointi 28 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine.

Care Boys itafunga msimu kwa kucheza na Espanyola Jumapili, mchezo ambao kama itafungwa au kutoka sare na Jaga ambayo itacheza na Swazi ikashinda, basi Care Boys itaondoshwa kwenye rada za kufukuzia nafasi ya pili.

Nyota wa Jaga, Hassan Ally alisema wao watacheza kutafuta pointi tatu, nani atakuwa wa pili hiyo itaamuliwa baada ya ligi kumalizika keshokutwa.

"Lengo letu ni kumaliza kwenye nafasi za juu, tutapambana kushinda Jumamosi, matokeo ya nafasi ya pili yako mikononi mwa mechi ya Espanyola na Care Boys.

Ligi hiyo itafikia tamati keshokutwa katika ngazi ya vituo ambavyo ilichezwa kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Ruvuma, Kilimanjaro, Iringa na Mwanza.

Meneja Masoko wa Betika, Nelson Mwanuzi alisema Ligi hiyo imefikia tamati kwa baadhi ya vito vya mikoa ikiwamo cha Iringa na Kilimanjaro.

"Mikoa ya Mwanza, Lindi, Ruvuma na Dar es Salaam inaelekea ukingoni ambapo tunatarajia ifikie tamati Mei 22 na baada ya apo timu zilizotwaa ubingwa zitachuana kwenye ngazi ya taifa," alisema.

# NBC Dodoma Marathon zaokoa wanawake

**Na Jumanne Juma**

JUMLA ya wanawake 9,000 wa hapa nchini wamepata nafasi ya kufanyiwa vipimo vya saratani ya shingo ya kizazi na wengine 550 waliogundulika wamepatiwa matibabu ya ugonjwa huo kupitia fedha zilizopatikana katika mbio za NBC Dodoma Marathon.

Hilo limewekwa wazi na Mkurugenzi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Theobald Sabi, wakati wa uzinduzi wa mbio za NBC Dodoma Marathon zitakazofanyika Julai 31 mwaka huu jijini Dodoma ikiwa ni msimu wa tatu.

Sabi alisema katika kuunga mkono juhudi za mapambano ya kansa ya kizazi kwa wanawake, NBC imeandaa marathon iitwayo 'NBC Dodoma Marathon' yenye lengo la kusaidia zaidi ya wanawake 20,000 wenye kansa ya kizazi.

Sabi alisema Tanzania pekee ndani ya mwaka mmoja zaidi ya wanawake 1,000 wanaopimwa wanagundulika kuwa na saratani ya kizazi.

Aliongeza kwa kipindi cha miaka miwili kwa kushirikiana na Hospitali ya Ocean Road wamefanikiwa kuwachunguza wanawake 9,000 na kati yao, 550 walipatiwa matibabu na wamepona ugonjwa huo.

Sabi aliongeza mwitikio wa washiriki katika mbio hizo ni mkubwa na mwaka huu wanatarajia kupata wanariadha 5,000 kutoka sehemu mbalimbali.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MANE ATAJWA PSG
KLABU ya Paris St-Germain ipo tayari kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30, huku kukiwa na ripoti kwamba amekwama katika mkataba wake mpya. Mkataba wa sasa wa Mane unamalizika Juni 2023. ***(Sport Bild)***

### PHILLIPS HUYO CITY
KLABU ya Manchester City ina nia ya kusajili kiungo wa kati wa Leeds United na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26, huku wakiangalia mtu wa kuziba nafasi ya Fernandinho mwenye umri wa miaka 37, ambaye anaondoka mwishoni mwa msimu huu baada ya miaka tisa. ***(Mirror)***

### MARTINEZ ATAKIWA MAN
KOCHA mpya wa Manchester United, Erik ten Hag amemwongeza, Lisandro Martinez mwenye umri wa miaka 24, kwenye orodha ya wachezaji anaowataka katika msimu huu. Martinez aliisaidia timu ya Ten Hag Jax kushinda ligi ya Uholanzi msimu wa 2021-22. ***(Telegraph)***

### SAVIC KWENYE RADA
MANCHESTER United pia wanamtaka kiungo wa kati wa Lazio, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 27, ambaye alifunga mabao 11 na asisti 11 katika mechi 36 za Ligi Kuu. ***(Calciomercato)***

### POGBA AWINDWA
PSG na Juventus zimeendelea kumuwinda kiungo wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake unamalizika mwisho wa msimu huu. ***(Fabrizio Romano)***

### ROMAGNOLI ATAKIWA CHELSEA
CHELSEA inataka kumsajili nahodha wa AC Milan, Alessio Romagnoli mwenye umri wa miaka 27 msimu huu katika uhamisho wa bila malipo. ***(Mundo Deportivo)***

### SANCHEZ AWANIWA LEICESTER
KLABU ya Leicester ipo tayari kumnunua mlinda mlango wa Hispania, ambaye kwa sasa anaichezea klabu ya Brighton, Robert Sanchez mwenye umri wa miaka 24, ambaye thamani yake ni pauni milioni 50, huku mlinda mlango wa Denmark, Kasper Schmeichel mwenye umri wa miaka 35, akiwa tayari kwa mazungumzo kuhusu mkataba mpya. ***(Telegraph)***

### PEPE AKASIRIKA
WINGA wa Arsenal, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 26 - ambaye alijiunga na klabu hiyo kwa gharama ya pauni milioni 72 mwaka 2019 - amekasirishwa na kukosa muda wa mechi na anaweza kulazimisha kuihama klabu hiyo. ***(Mirror)***

### JESUS SAFI ARSENAL
ARSENAL inatarajia kuweka dau la pauni milioni 35 kwa mshambuliaji wa Manchester City, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 25, ambaye amepanga kuondoka baada ya kuwasili kwa Erling Haaland. ***(football.london)***

### GALLAGHER, BROJA KURUDI
KIUNGO wa kati wa England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 22, na mshambuliaji wa Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 20, watarudi Chelsea wakati mikopo yao kule Crystal Palace na Southampton itakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Fabrizio Romano)***

***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG ASTAAFU KUITUMIKIA NCHI YAKE

Ni timu ya Taifa ya Gabon ambayo katika AFCON mwaka huu...

**BARCELONA, Hispania**

MSHAMBULIAJI Pierre-Emerick Aubameyang amestaafu soka la kimataifa, Shirikisho la Mpira wa Miguu la Gabon limesema.

Shirikisho hilo lilisema lilipokea barua kutoka kwa mshambuliaji huyo wa Barcelona na nahodha wa Gabon, Jumanne akiarifu kuhusu uamuzi wake, baada ya kuichezea timu hiyo kwa miaka 13.

Gabon lilichapisha sehemu ya barua ya Aubameyang, ambapo aliwashukuru watu wa Gabon, makocha wake, wachezaji wenzake na baba yake, ambaye pia aliichezea Gabon katika miaka ya 1980 na 1990.

"Natumaini kumenifanya nijivunie kwa kuvaa jezi za rangi zetu," Aubameyang aliandika katika barua yake.

Aubameyang mwenye umri wa miaka 32 aliichezea Gabon mara 72 na ndiye mfungaji bora wa muda wote wa nchi yake akiwa na mabao 30.

Aubameyang akiwa kitovu cha timu, Gabon ilifika robo fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2012 ikiwa ndio nafasi kubwa zaidi waliyofikia kwenye mashindano ya kimataifa.

Michuano ya mwisho kwa Aubameyang akiwa na Gabon ilikuwa michungu kwani alipoambukizwa COVID-19 mwanzoni mwa Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka huu nchini Cameroon na ikabidi ajiondoe kwenye mashindano hayo bila kucheza mchezo wowote.

Ametangaza uamuzi wake wa kustaafu kucheza mechi za kimataifa wiki mbili kabla ya Gabon kuanza kampeni ya kufuzu Kombe la Mataifa ya Afrika mwakani nchini Ivory Coast.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 200,

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
BETIS
1 | 1.74
X | 4.03
2 | 4.03

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TUCHEL ATAKA CHELSEA IUZWE HARAKA




**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel amesema anatumaini uuzwaji wa klabu hiyo utafanikiwa "haraka iwezekanavyo".

The Blues hao walifikia makubaliano ya mauzo ya klabu kwa kundi la umiliki linaloongozwa na Todd Boehly, Clearlake Capital, Mark Walter na Hansjorg Wyss kwa kiasi cha pauni bilioni 4.25 mapema Mei.

Ununuaji huo ambao unaahidi uwekezaji wa pauni bilioni 1.75 katika klabu hiyo, ulitarajiwa kukamilishwa mwishoni mwa mwezi huu, lakini ripoti za hivi karibuni zimeeleza Roman Abramovich anaweza kukwepa mpango huo kwa kukataa muundo wa mauzo.

Akizungumza katika mkutano na wanahabari kuelekea mchezo wa Chelsea dhidi ya Leicester jana, Tuchel alitaka mambo yakamilike mapema kuliko baadaye.

Alisema: "Ninafahamu ilivyo, lakini sina habari mpya. Sijafahamishwa kuhusu tabia ya masuala ambayo yamefika. Kwa hiyo tusubiri.

"Bado nina hakika kuwa iko mikononi mwangu, sio mikononi mwangu. Tunatumaini itapitia haraka iwezekanavyo."

Chelsea walipoteza kwa huzuni fainali ya Kombe la FA Jumamosi kwa Liverpool kwa mikwaju ya penalti, pia akifungwa kwenye fainali ya Kombe la Carabao, Februari.

# Pogba azigonganisha Juventus, PSG

**PARIS, Ufaransa**

KIUNGO nyota wa Manchester United ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto, Paul Pogba amefanya mazungumzo na klabu mbili kuhusu uwezekano wa kuondoka pale Old Trafford.


Pogba mwenye umri wa miaka miaka 29 ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu amepanga kufungasha virago vyake kuondoka pale viunga vya Old Trafford.

Huku kukiwa na taarifa za hivi karibuni zikimhusisha kuhamia kwenye klabu ya Manchester City.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mirror, Pogba anatarajiwa kujiunga na timu moja wapo kati ya Juventus au PSG kwenye majira ya joto, kutokana na kufungua uwanja wa mazungumzo na klabu hizo mbili.

Kuna taarifa zinasema PSG imemwekea kiasi cha pauni 350,000 kama mshahara wake kwa wiki ili kujiunga na mabingwa hao wa Ufaransa.

Lakini Juventus haiwezi kuondolewa japo imetenga kiasi kidogo cha mshahara wake sababu amekuwa Turin kwa muda na kucheza kwa mafanikio hapo.



## HABARI MICHEZO

,000,000

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/05/22 | 18:00 | Crystal Palace vs Manchester Utd | 2.89 | 3.32 | 2.31 |
| 02. 22/05/22 | 18:00 | Brentford vs Leeds | 2.28 | 3.42 | 2.87 |
| 03. 22/05/22 | 18:00 | Burnley vs Newcastle | 2.34 | 3.22 | 2.92 |
| 04. 22/05/22 | 18:00 | Brighton vs West Ham | 2.45 | 3.30 | 2.71 |
| 05. 22/05/22 | 18:00 | Brondby vs Silkeborg | 2.48 | 3.59 | 2.54 |
| 06. 22/05/22 | 18:30 | Kalmar vs Djurgardens IF | 2.77 | 2.97 | 2.48 |
| 07. 22/05/22 | 18:30 | Elche vs Getafe | 3.05 | 2.95 | 2.49 |
| 08. 22/05/22 | 19:00 | Stromsgodset vs Valerenga | 2.64 | 3.29 | 2.54 |
| 09. 22/05/22 | 19:00 | Jerv vs Odd Ballklubb | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 10. 22/05/22 | 21:00 | Ham-Kam vs Rosenborg | 2.53 | 3.27 | 2.68 |
| 11. 22/05/22 | 23:00 | Real Sociedad vs Atletico Madrid | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 12. 22/05/22 | 23:00 | Barcelona vs Villarreal | 2.47 | 3.60 | 2.58 |
| 13. 22/05/22 | 23:00 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.35 | 3.35 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
“1” - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
“X” - NI TIMU KUTOKA SARE
“2” - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 20/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1201 | Coastal Union vs Dodoma FC | 2.17 | 2.77 | 3.59 |
| 15:30 | 2174 | Genoa Youth vs Napoli Youth | 1.94 | 3.40 | 3.44 |
| 16:00 | 1044 | Namungo vs Tanzania Prisons | 2.11 | 2.85 | 4.10 |
| 17:00 | 3472 | Boluspor vs Altinordu | 1.59 | 3.84 | 4.77 |
| 17:00 | 3782 | Tuzlaspor vs Samsunspor | 2.59 | 3.32 | 2.43 |
| 18:00 | 1614 | CSKA Moscow Youth vs Rostov Youth | 1.40 | 4.47 | 6.21 |
| 18:00 | 2072 | Dinamo Moscow Youth vs Lokomotiv Moscow Youth | 3.00 | 3.49 | 2.08 |
| 18:00 | 2753 | Kryliya Sovetov Youth vs Zenit Youth | 6.80 | 4.90 | 1.39 |
| 18:00 | 5036 | Spartak Moscow Youth vs Chertanovo Moscow Youth | 1.46 | 4.37 | 5.43 |
| 18:00 | 5107 | Znojmo vs Banik Ostrava B | 3.27 | 4.59 | 1.74 |
| 18:00 | 5738 | FC Minsk vs Shakhter Soligorsk | 5.84 | 3.89 | 1.49 |
| 18:30 | 1499 | Japs vs FC KTP | 4.08 | 3.79 | 1.69 |
| 18:30 | 3628 | Mladost Lucani vs Spartak Subotica | 1.63 | 3.58 | 4.84 |
| 18:30 | 3898 | Proleter vs Novi Pazar | 3.07 | 2.97 | 2.28 |
| 18:30 | 5964 | FK Radnicki 1923 vs Metalac | 2.18 | 3.10 | 3.50 |
| 19:00 | 1468 | Istra vs Slaven Belupo | 2.42 | 3.20 | 2.67 |
| 19:00 | 5212 | Jiskra Domazlice vs Karlovy Vary | 1.53 | 4.27 | 4.66 |
| 19:30 | 1811 | Athletic Youssoufia vs FAR Rabat | 4.50 | 3.05 | 1.92 |
| 20:00 | 1019 | LASK Linz vs Admira Wacker | 1.68 | 3.69 | 4.27 |
| 20:00 | 1243 | Lokomotiv Plovdiv vs CSKA 1948 | 3.11 | 3.20 | 2.15 |
| 20:00 | 1625 | TSV Hartberg vs Josko Ried | 2.87 | 2.18 | 3.41 |
| 20:00 | 1731 | Denizlispor vs Erzurum BB | 3.21 | 3.50 | 1.99 |
| 20:00 | 2543 | B 1913 Odense vs BK Marienlyst | 2.90 | 3.70 | 2.21 |
| 20:00 | 2853 | Balikesirspor vs Eyupspor | 13.66 | 6.63 | 1.14 |
| 20:00 | 3131 | Arda Kurdzhali vs Beroe | 3.50 | 3.31 | 1.95 |
| 20:00 | 4348 | Istanbulspor vs Bandirmaspor | 2.86 | 3.35 | 2.21 |
| 20:00 | 4923 | Gaziantep BB vs Caykur Rizespor | 1.82 | 3.74 | 3.89 |
| 20:00 | 5279 | Antalyaspor vs Galatasaray | 2.22 | 3.52 | 2.93 |
| 20:00 | 5994 | SCR Altach vs WSG Wattens | 1.57 | 4.08 | 4.56 |
| 20:30 | 5486 | Universitatea Craiova vs Farul Constanta | 2.11 | 3.32 | 3.27 |
| 21:00 | 1916 | Thor Akureyri vs UMF Grindavik | 2.77 | 3.79 | 2.11 |
| 21:05 | 3998 | Lokomotiva Zagreb vs HNK Sibenik | 1.48 | 4.18 | 5.44 |
| 21:30 | 2622 | AJ Auxerre vs Sochaux | 2.08 | 3.14 | 3.63 |
| 21:30 | 3935 | Cosenza vs Vicenza | 2.46 | 3.07 | 2.87 |
| 21:30 | 4373 | Kaiserslautern vs Dynamo Dresden | 2.04 | 3.36 | 3.56 |
| 21:30 | 5206 | AC Reggiana vs Feralpisalo | 2.05 | 3.21 | 3.31 |
| 21:45 | 2303 | St Patricks vs Shelbourne | 1.75 | 3.40 | 4.27 |
| 21:45 | 2777 | Inverness vs St Johnstone | 2.63 | 3.03 | 2.73 |
| 21:45 | 3562 | Drogheda Utd vs Finn Harps | 2.58 | 3.02 | 2.63 |
| 21:45 | 3642 | Cork City vs Wexford Youths | 1.30 | 5.06 | 7.39 |
| 21:45 | 3676 | Derry City vs Dundalk FC | 1.68 | 3.60 | 4.38 |
| 21:45 | 3698 | Bohemians FC vs Sligo Rovers | 1.98 | 3.36 | 3.36 |
| 21:45 | 3778 | Galway United vs Athlone Town | 1.15 | 6.58 | 12.58 |
| 21:45 | 4502 | Treaty United vs Cobh Ramblers | 1.76 | 3.55 | 3.99 |
| 21:45 | 4897 | Torino vs Roma | 3.42 | 3.57 | 1.97 |
| 22:00 | 2294 | Rayo Vallecano vs Levante | 1.95 | 3.80 | 3.40 |
| 22:00 | 2605 | Real Madrid vs Betis | 1.74 | 4.03 | 4.03 |
| 22:00 | 4605 | Zaragoza vs Lugo | 2.05 | 3.26 | 3.51 |
| 22:15 | 1434 | Kordrengir vs KV Vesturbaer | 1.51 | 4.48 | 4.67 |
| 22:15 | 2154 | Afturelding vs UMF Selfoss | 2.73 | 3.85 | 2.11 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MBEYA KWANZA YAIHOFIA YANGA IKIMWOTA MAKATA

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Mbeya Kwanza umesema mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya vinara Yanga, utakuwa mgumu huku wakimkosa mchezaji wao muhimu, Enock Jiah ambaye alionyeshwa kadi nyekundu katika mechi iliyopita.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Mbeya Kwanza, Mohamed Mashango, alisema mchezo utakuwa na ushindani kwa sababu wao ni wageni na wanashiriki mara ya kwanza Ligi Kuu Tanzania Bara.

“Mchezo utakuwa mgumu, tunafahamu tunakwenda kukutana na timu ambayo haijafungwa mpaka sasa, vilevile ina kikosi kipana hivyo lazima tuingie kwa tahadhari,” alisema Mashango.

Mwenyekiti huyo alisema kikosi chake kinaendelea na mazoezi ya mwisho kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo na anaamini wachezaji wakifuata vyema maelekezo ya benchi ya ufundi watapata matokeo mazuri. Alisema baada ya aliyekuwa Kocha wao mkuu, Mbwana Makata kufungiwa kutojihusisha na mpira kwa muda wa miaka mitano, uamuzi huo umewaathiri kwa kiasi kikubwa wachezaji pamoja na benchi zima la ufundi.

“Taarifa hiyo imetuathiri sisi pamoja na benchi zima la ufundi, baada ya michezo yetu miwili tutafanya mpango wa kumtafuta mbadala wa Makata isipokuwa kwa sasa timu ipo chini ya kocha wetu msaidizi,” Mashango alisema.

Makata alipata adhabu hiyo baada ya kubainika kuwashawishi wachezaji kugomea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo iliyopangwa kuchezwa Ijumaa iliyopita kwa madai hakuna gari la wagonjwa.

Kiongozi mwingine wa timu hiyo aliyekumbana na adhabu ya kifungo ni meneja, David Naftali.

Tayari Namungo FC imepewa pointi tatu na mabao matatu kufuatia wageni Mbeya Kwanza kugomea mchezo huo uliotarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Mbeya.



Baadhi ya wateja na mashabiki wakishiriki katika matukio ya shamrashamra za kuelekea kuwasili kwa ziara ya Kombe Halisi la Dunia la FIFA nchini Tanzania kwa kushirikiana na Coca-Cola, jijini Arusha jana. Kombe hilo linatarajiwa kuwasili katika Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam Mei 31 mwaka huu, ambapo litapelekwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan na kulipokea na kulishika kwa niaba ya Watanzania wote. Wateja na mashabiki wa soka nchini watapata fursa ya kuliona kwa karibu na kupiga nalo picha Juni 1, 2022 katika Uwanja wa Benjamini Mkapa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nchemba, klabu zapanga mikakati

**Na Scola Malinga, WFM**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amekutana na klabu za michezo pamoja na taasisi za serikali zinazosimamia sekta hiyo ili kujadili mipango na mikakati ya kuendeleza sekta ya michezo nchini.

Wadau hao walimweleza Nchemba kuhusu changamoto wanazokutana nazo katika kuendeleza soka ikiwamo ufinyu wa bajeti katika vilabu vyao pamoja na kuiomba serikali iendelee kutoa nafuu zaidi ya kodi kwenye nyasi bandia pamoja na viunganishi vyake.

Dk. Nchemba amewahakikishia wadau hao maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyowapa ni kuhakikisha sekta ya michezo inakuzwa kwa kuwa ni muhimu na vijana wengi wamejiajiri kupitia sekta hiyo.

Alitoa wito kwa vyama vinavyosimamia michezo nchini kuhakikisha sekta hiyo inafanya vizuri ili kupeperusha vyema bendera ya Tanzania ndani na nje ya nchi pamoja na kuhakikisha miundombinu ya viwanja inajengwa kwenye maeneo ya kimkakati ili kukuza michezo nchini.

Akizungumza kwa niaba ya vilabu hivyo vya mpira wa miguu nchini, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi na Makamu wa Pili wa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Steven Mnguto aliishukuru serikali kwa kuthamini michezo na kuomba changamoto walizoziwasilisha kwake zifanyiwe kazi ili soka la hapa nchini lipige hatua zaidi na kuzipa nafuu klabu ili zijiendesha vizuri.

Michezo
Ijumaa Mei 20, 2022
Nipashe





Aubameyang astaafu kuitumikia nchi yake



Kipa wa Simba, Aishi Manula (aliyelala chini), akifanikiwa kudaka moja ya mashambulizi langoni mwake katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam juzi usiku. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA YAITISHA MBEYA KWANZA

●●●Yatamba itatumia nguvu ile ile kwa sababu inahitaji ushindi na...

**Na Saada Akida**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanatarajia kuwakaribisha Mbeya Kwanza kutoka Mbeya katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa leo kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Awali mchezo huo ulipangwa kuchezwa kesho lakini ukarudishwa nyuma siku moja kutokana na mabadiliko yaliyotolewa katika ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Yanga itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji wakati Mbeya Kwanza yenyewe ilifungwa goli 1-0 na Geita Gold, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Majimaji Mjini Songea.

Enock Jiah wa Mbeya Kwanza anatarajiwa kukosekana kwenye mchezo huo baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu kwenye mchezo uliopita dhidi ya Geita Gold. Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, alisema mechi hiyo ni mechi ya kawaida lakini wanatakiwa kujiandaa zaidi kwa sababu timu zilizoko mkiani hucheza kwa kukamia pale wanapokutana na vigogo.

Nabi alisema watacheza kwa tahadhari kubwa katika mchezo huo kwa sababu hataki kurudia kile kilichotokea walipokutana na Tanzania Prisons ambapo waligawana pointi.

"Tunajua tunaenda kucheza na timu ambayo iko chini na wanahitaji kupata matokeo mazuri ili kujiweka sehemu salama dhidi ya janga la kushuka daraja, lakini upande wetu tunahitaji pointi tatu ili kujiweka imara katika mbio za kuwania ubingwa wa ligi hii," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema katika mchezo huo kutakuwa na mabadiliko kwenye kikosi chake kwa sababu anahitaji kutoa nafasi kwa kila mchezaji kwenye michezo iliyobakia na kusaidia timu yao.

"Suala la ubingwa bado Yanga haijakuwa bingwa, akili zote tunaumiza kichwa katika mechi zilizoko mbele yetu hasa ukizingatia ndani ya siku tisa kuna mechi tatu, lazima kuwepo na mabadiliko ya kikosi, wengine tutawapa mapumziko kwa ajili ya mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA," Nabi alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Mbeya Kwanza, Aswile Asukile, alisema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanakuwa timu ya kwanza kuifanyia maajabu Yanga.

"Mchezo utakuwa mgumu kwa sababu Yanga iko vizuri, suala la kutokuwapo benchi kwa kocha wetu mkuu (Mbwana Makata), hatujaathirika na mipango yetu ya kutafuta pointi katika mchezo huu dhidi ya Yanga," alisema Aswile.

Nahodha wa Mbeya City, Mohammed Kapeta, alisema: "Tumejiandaa vizuri na tunatambua Yanga iko vizuri, hawajapoteza mechi na tunaenda kupambana kutafuta pointi katika mchezo huo."

Mbeya Kwanza inaburuza mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 21 huku timu nyingine iliyoko kwenye janga hilo la kushuka daraja ni Tanzania Prisons na Biashara United.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitaendelea tena kesho kwa Mtibwa Sugar kuikaribisha Azam FC kwenye Uwanja wa Manungu ulioko Turiani, Morogoro wakati Ruvu Shooting itawafuata Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba Mjini Bukoba.

## Simba yakubali mambo mazito

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, akisema mechi yao dhidi ya Azam FC ilikuwa ngumu, mabosi wa klabu hiyo wamesema akili na nguvu zao zote ni kuhakikisha wanatetea ubingwa wa Kombe la FA msimu huu.

Pablo alisema matokeo ya sare ni ya kawaida katika mchezo wa soka lakini alibainisha mechi hiyo ya juzi ilikuwa na ushindani kwa sababu timu zote zinashabihiana uwezo na kipindi cha pili wachezaji wake walionyesha kiwango bora.

"Mchezo ulikuwa mgumu ingawa kuna nafasi ambazo tulipata tukashindwa kuzitumia, kipindi cha pili wachezaji walicheza kwa nguvu na kwa ubora wa hali ya juu," alisema Franco.

Alisema anajipanga kukutana na Geita Gold na kuongeza anaiheshimu timu hiyo kutokana na kuwa na wachezaji wazuri.

"Matokeo ya sare dhidi ya Azam sio rafiki kwetu katika mbio za kutetea ubingwa wa wa Ligi Kuu Tanzania, ni matokeo ambayo hatukusudia kupata, tulihitaji kuondoka na pointi zote tatu ambazo zingetufanya kupunguza tofauti ya pointi na wanaoongoza ligi," Pablo alisema.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally alisema matokeo waliyopata dhidi ya Azam FC si mazuri lakini wanayaheshimu kwa sababu wachezaji wao walipambana.

"Tumekosa ushindi dhidi ya Azam FC, malengo na dhamira yetu ya ubingwa imekuwa ngumu na sasa nguvu zetu kubwa tunazielekeza katika Kombe la ASFC huku tukiendelea kupambana kutafuta pointi katika michezo sita iliyobakia katika ligi," alisema na aliongeza;

"Kwa hali tuliyokuwapo na kwa matokeo haya malengo ya ubingwa yamezidi kuwa magumu kwa sababu ili Simba iwe bingwa lazima kushinda mechi zote na lazima wapinzani wetu wapoteze na kufanya vibaya jambo hilo ni ngumu kulingana na msimu huu kutokuwa vizuri," alisema Ahmed Ally.

Simba inatarajia kusafiri kwenda Mwanza kuwafuata Geita Gold FC katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >